JAMHURI YA KENYA
WIZARA YA ELIMU

# MTAALA WA SHULE YA MSINGI

# KISWAHILI

# GREDI YA 5

# KWA WANAFUNZI WALIO NA CHANGAMOTO ZA KUONA

**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**
***JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI***

Chapisho laKwanza 2017
Chapisho la Pili 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

ISBN: 978-9914-43-826-0
Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

## UTANGULIZI

Serikali ya Kenya inajitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera kuhusu elimu, mafunzo, na utafiti yanakidhi matarajio ya Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya Kenya 2030, Sera ya Mtaala wa Kitaifa ya 2019, Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs), na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Kenya imesaini. Kuelekea kufikia lengo la Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu (MoE) imetekeleza kwa mafanikio na hatua kwa hatua utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi (CBC) katika ngazi ya awali, msingi, na Shule za Upili za daraja la chini.

Utekelezaji wa Mtaala wa Kitaalamu unajumuisha ufuatiliaji na tathmini ili kubaini mafanikio yake. Baada ya mzunguko wa miaka mitano wa utekelezaji, tathmini ya jumla ya mzunguko wa elimu ya msingi ilifanywa ili kubaini kufikia malengo ya matokeo ya kujifunza kama ilivyotarajiwa katika Mfumo wa Mtaala wa Elimu ya Msingi.

Serikali ya Kenya iliunda Jopo Kazi la Rais kuhusu Mageuzi ya Elimu'Presidential working party on Education Reforms' (PWPER) mwaka 2022 kushughulikia masuala muhimu yanayoathiri sekta ya elimu. PWPER ilifanya mapendekezo ya mbalimbali, yaliyochangia marekebisho ya mtaala. Mapendekezo ya PWPER, ripoti za ufuatiliaji, tathmini ya jumla, maoni kutoka kwa watekelezaji wa mtaala, na wadau wengine, yalisababisha hatua ya kufanya marekebisho katika mtaala pamoja na kuchunguza upya masomo yaliyopendekezwa.

Mtaala wa Gredi ya **5** kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona uliofanyiwa marekebisho, umejengwa kutokana na umilisi uliokuzwa katika Gredi ya **4**. Umuhimu katika gredi hii ni maendeleo ya usomaji wa msingi, hesabu, na stadi za mwingiliano na mazingira.

Mitaala hii inawakilisha Malengo ya Kitaifa ya Elimu, kauli kiini, matokeo yanayotarajiwa kwa ujumla na kwa kila somo pamoja na Mada na Mada Ndogo. Mitaala hiyo pia inajuimuisha Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa. Swali Dadisi Lililopendekezwa, Umilisi wa kimsingi unaokuzwa: masuala mtambuko(PCI's), maadili, vigezo na viwango vya kuzingatia katika kutathmini.

Ni matumaini yangu kuwa mashirika yote ya serikali na wadau wengine katika Elimu watatumia miundo hii ili kuwezesha ufanisi na utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika kiwango hiki.

**HON. EZEKIEL OMBAKI MACHOGU, CBS**
**WAZIRI IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

**DIBAJI**

Wizara ya Elimu (MoE) ilianza kutekeleza Mtaala wa Kiumilisi (CBC) mwaka 2019 nchini kote. Gredi ya Kwanza ndiyo ya kwanza katika ngazi ya Elimu ya Msingi nayo Gredi ya Sita ni ya mwisho katika ngazi hiyo katika mfumo uliofanyiwa marekebisho wa elimu.

Mtaala uliofanyiwa marekebisho wa Gredi **ya 5** unaendeleza utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi kutoka Gredi ya **4** katika ngazi ya Msingi. Mtaala huu unatoa fursa kwa wanafunzi kuzingatia wanachokipenda ili kuunda msingi wa elimu na mafunzo zaidi na/au kupata stadi za ajira. Kiwango hiki cha elimu ni muhimu sana katika kuchangia kufikia ruwaza na mwito wa marekebisho yanayoendelea ya kimtaala kama ilivyoelekezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 kuhusu Kuelekea kuafikia elimu na mafunzo yenye ubora, faafu na jumuishi kwa maendeleo endelevu nchini Kenya ''*Towards Realizing Quality, Relevant and Inclusive Education and Training for Sustainable Development'*. Mswada Elekezi huo unaeleza kuhusu kuvuka kutoka mtaala wa Kimafunzo na kuzingatia kukuza vipawa vya kila mwanafunzi.

Hivyo basi, mtaala wa Gredi ya **5** kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona inalenga kuimarisha ukuzaji wa Umilisi wa Kimsingi katika mtaala huu, yaani: mawasiliano na ushirikiano, uwazaji kina na utatuzi wa matatizo, ubunifu, uraia, ujuzi wa kidijitali, hamu ya kuendelea kujifunza na kujiamini.

Mitaala inapendekeza shughuli shirikishi za ujifunzaji unaolingana na Mada Ndogo mbalimbali na vipengele vingine vya mtaala wa umilisi (CBC). Pia inapendeza baadhi ya nyenzo za kufundishia na mbinu za kutathmini mbalimbali. Inatarajiwa kwamba mitaala hii itaongoza walimu kufanikisha wanafunzi kufikia matokeo maalum yanayotarajiwa ya kujifunza katika Gredi ya **5** na kuwaandaa kwa mpito laini kwa Gredi ya **6**. Ni matumaini yangu kuwa mwalimu atatumia mitaala iliyorekebishwa kufanya ujifunzaji uwe wa kuvutia, unaochangamsha na wa kufurahiwa.

**DKT. BELIO KIPSANG', CBS**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

## SHUKRANI

Sheria Nambari 4 ya 2013 (Toleo jipya 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (KICD) inaipa uwezo Taasisi kukuza na kufanyia marekebisho *(SNE adapt)* na vifaa vya msaada kwa mtaala kwa elimu ya msingi na ya vyuo vya Elimu na Mafunzo ya juu vilivyo chini ya vyuo vikuu. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote huhusisha utafiti, ulinganishi wa kimataifa, na uhusishaji mkubwa wa wadau. Kupitia kwa mchakato huu wa utaratibu na wa mashauriano, KICD ilizua wazo la Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) 2017 ambao unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Itifaki ya Jumuia ya Afrika Mashariki na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. (SGDs).

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (KICD) hufadhiliwa na Serikali ya Kenya ili kutekeleza majukumu na mipangilio ya serikali na sekta ya elimu. Pia, Taasisi hupata msaada kutoka kwa mashirika mengine ya kimaendeleo yanayoangazia miradi teule.

Mtaala uliyorekebishwa Gredi ya 4 kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona ilipangwa na kubadilishwa kwa msaada wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Usawa wa Elimu ya Msingi ya Kenya katika Programu ya Kujifunza ‘Kenya Primary Education Equity in Learning Programme’ (KPEELP): mradi ulioratibiwa na MoE. Kwa hiyo, Taasisi inashukuru sana kwa msaada wa Serikali ya Kenya, kupitia MoE, na washirika wa maendeleo kwa msaada wa sera, rasilimali, na msaada wa logistiki. Kwa namna ya pekee, shukrani maalum kwa Waziri wa Elimu-MoE na Katibu Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi.

Ningependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wanaelimu wengine walioshiriki kama wanajopo katika ukuzaji wa mitaala. Nashukuru pia mashirika mengine yanayoshirikiana na serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali kwa majukumu mbalimbali waliyotekeleza katika ukuzaji na ubalishaji wa Mitaala ya Gredi ya 4-6 kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona. Kuhusiana na hili, ningependa kushukuru Katibu wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Kitaifa la Mitihani (KNEC) kwa msaada wao katika mchakato wa kukuza na kubadilisha mitaala hii. Mwisho, ninawashukuru sana mwenyekiti wa baraza la KICD na wanachama wengine wa Baraza kwa mwongozo thabiti katika mchakato huu.

Nawahakikishia watekelezaji wa mtaala, wazazi na washikadau wengine kuwa mitaala hii itaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya **5** na maandalizi ya wanafunzi walio na changamoto za kuona kwa mpito wa Gredi ya **6**.

**PROF. CHARLES O. ONG’ONDO, MBS**
**MKURUGENZI/OFISA MTENDAJI**
**MKUU TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

**YALIYOMO**

UTANGULIZI ... ii

DIBAJI ... iii

SHUKRANI ... iv

YALIYOMO ... v
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ... vi
MGAO WA VIPINDI KATIKA SHULE YA MSINGI ... viii
MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA ELIMU YA MSINGI ... ix
MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI ... xi
1.0 MAPISHI ... 14
2.0 HUDUMA YA KWANZA ... 29
3.0 MAPAMBO ... 40
4.0 SAA NA MAJIRA ... 54
5.0 KUKABILIANA NA UMASKINI ... 66
6.0 MAADILI ... 71
7.0 ELIMU YA MAZINGIRA ... 81
8.0 NDEGE WA PORINI ... 92
9.0 MAGONJWA ... 102
10.0 KUDHIBITI ITIKADI ZA KIDINI NA ZA KIJAMII ... 110
11.0 UWEKEZAJI ... 129
MWONGOZO WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA ... 136
KIAMBATISHO 1: MWONGOZO WA MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI KATIKA GREDI YA 4-6 ... 142
KIAMBATISHO 2: MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI ... 145

**MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA**

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.

   a) **Mahitaji ya kijamii**
      Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**
      Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
      Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda. Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
   Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa.
   Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
   Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
   Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

**MGAO WA VIPINDI KATIKA SHULE YA MSINGI**

| S/ No. | Somo | Vipindi |
|---|---|---|
| 1. | English for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 2. | Kiswahili for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 3. | Mathematics for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 4. | Religious Education | 3 |
| 5. | Science & Technology for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 6. | Agriculture & Nutrition for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 7. | Social Studies for Learners with Visual Impairment | 3 |
| 8. | Creative Arts for Learners with Visual Impairment | 6 |
| 9. | Pastoral/ Religious Instruction Programme | 1 |
| | **Jumla** | **35** |

## MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA ELIMU YA MSINGI

Kufikia mwisho wa elimu ya msingi, mwanafunzi aweze:

a) kuwasiliana apasavyo akitumia mbinu za mazungumzo na ishara katika miktadha mbalimbali,
b) kutumikiza maarifa, ujuzi, maadili na mitazamo katika maisha ya kila siku,
c) kudhhihirisha ujuzi wa kijamii maadili, na maadili ya kidini kwa nia ya kuchangia kukua kwa jamii,
d) kukuza talanta kwa nia ya kujiendeleza na kujifanikisha,
e) kuafiti, kutumia, kulinda na kutunza mazingira kwa nia ya kujifunza na kwa maendeleo endelevu,
f) kutumia ujuzi wa kidijitali kujifunza na kujifurahisha,
g) kuthamini tamaduni mbalimbali kwa nia ya kuishi kwa amani,
h) kufurahia haja ya umuhimu wa kutegemeana kwa binadamu na mataifa.

## KAULI KIINI

Mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili aliye na changamoto za kuona katika shule ya msingi atajenga stadi na umahiri ufaao kuwasiliana, kutangamana na kushiriki katika miktadha mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kutumia lugha kuzungumza na kuandika. Mwanafunzi aliye na changamoto za kuona anahitaji kujifunza kunga za Kiswahili ili kuitumia lugha hii kama wenzo wa ujifunzaji. Mwanafunzi asiyeona, pia anahitaji kujifunza kutumia alama za breli zifaazo na mikato ya breli ili kuimarisha uwezo wao wa kuandika na kusoma. Aidha, mwanafunzi hufunzwa Kiswahili ili kushiriki na kukichangamkia katika hali zake mbalimbali. Hili humwezesha kujenga stadi za kimsingi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kwa kujifunza sarufi na matumizi ya Kiswahili kimuktadha, mwanafunzi anaweza kuwasiliana kwa ufasaha, umahiri na kwa namna ambayo itaimarisha utangamano darasani na katika ulimwengu mpana. Nadharia ya sarufi bia ya Noam Chomsky (1965), inaeleza kuwa binadamu ana uwezo asilia wa kuvimudu vipengele vya kisarufi. Uwezo huu huchangia katika ukuaji wa lugha wa mwanafunzi na hivyo kumfanya mzungumzaji stadi wa lugha anayeweza kubaini matumizi sahihi na yasiyo sahihi.

**MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI**

Kufikia mwisho wa Shule ya Msingi, mwanafunzi aweze:

a) kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano,

b) kuzingatia kanuni za lugha kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi,

c) kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali,

d) kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti maishani,

e) kutumia hati au nukta nundu zifaazo za kimaandishi na mfumo wa kidijitali wenye teknolojia saidizi kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali,

f) kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku.

**MADA**

1. Kusikiliza na Kuzungumza
2. Kusoma
3. Kuandika
4. Sarufi MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Muda Uliopendekezwa** |
|---|---|---|
| **Kusikiliza na Kuzungumza** | 1.1.1 Matamshi Bora (Sauti f/v, s/z, l/r/ na th/dh) | 2 |
| | 2.1.1 Maamkuzi na Maagano | 2 |
| | 3.1.1 Vitendawili | 2 |
| | 4.1.1 Heshima Adabu na Vyeo | 2 |
| | 5..1 Methali | 2 |
| | 6.1.1Ushairi | 2 |
| | 7.1.1 Nahau | 2 |
| | 8.1.1Visawe | 2 |
| | 9.1.1.1Mazungumzo ya Kimuktadha | 2 |
| | 10.1.1 Tashbihi | 2 |
| | 11.1.1 Masimulizi | 2 |
| **Kusoma** | 1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 2.2.1 Kusoma kwa Kina | 3 |
| | 3.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |
| | 4.2.1Kusoma kwa Mapana | 2 |
| | 5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 6.2.1Kusoma kwa Mapana | 2 |
| | 7.2.1 Kusoma kwa Mapana | 3 |
| | 8.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 3 |
| | 9.2.1 Kusoma kwa Mapana | 3 |
| | 10.2.1. Kusoma Kidijitali | 2 |
| | 11.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| **Kuandika** | 1.3.1 Insha ya Wasifu, | 2 |
| | 2.3.1 Insha ya Masimulizi | 2 |
| | 3.3. Kuandika kwa Tarakilishi | 2 |
| | 4.3.1 Baruapepe | 2 |
| | 5.3.1 Insha za Maelezo | 2 |
| | 6.3.1 Insha za Masimulizi | 2 |
| | 7.3.1 Insha za Maelezo | 2 |
| | 8.3.1 nsha za Masimulizi | 2 |
| | 9.3.1 Kuandika Maelezo | 2 |
| | 10.3.1 Insha za Masimulizi | 2 |
| | 11.3.1 Baruapepe | 2 |
| **Sarufi** | 1.4.1 Nomino za Pekee. | 2 |
| | 1.4.2 Nomino za Kawaida | 2 |
| | 2.4.1 Nomino za Wingi | 2 |
| | 2.4.2 Vitenzi Jina | 2 |
| | 3.4.1 Nomino za Makundi | 2 |
| | 3.4.2 Nomino Ambata | 2 |
| | 3.4.3 Nomino Dhahania | 2 |
| | 3.4.4Uakifishaji | 4 |
| | 4.4.1 Ngeli ya I-ZI | 4 |
| | 5.4.1 Ngeli ya U-ZI | 4 |
| | 6.4.1 Ngeli ya U-YA | 4 |
| | 7.4.1 Ngeli ya KU-KU | 4 |
| | 8.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi | 2 |
| | 9.4.1 Vinyume vya Vitenzi | 2 |
| | 10.4.1 Nyakati na Hali | 2 |
| | 11.4.1 Ukanushaji | 2 |
| | 11.4.2. Ukubwa na Udogo wa Nomino | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 11.4.3 Udogo wa Nomino | 2 |
| | **Jumla ya Vipindi** | **120** |

**1.0 MAPISHI**

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Matamshi Bora**<br><br>Sauti f/v, s/z, l/r/ na th/dh<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno: f/v, s/z, l/r na th/dh,<br>b) kutamka silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi: f/v, s/z, l/r na th/dh ili kutofautisha matamshi yake,<br>c) kutamka vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi: f/v, s/z, l/r na th/dh ili kuimarisha mawasiliano,<br>d) kutunga vitanzandimi vyenye maana | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno: f/v, s/z, l/r na th/dh.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana<br>● kimatamshi: f/v, s/z, l/r na th/dh ili kutofautisha matamshi yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti | 1. Unawezaje kutambua silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno?<br>2. Je, vitanzandimi hutamkwa vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kutokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi: f/v, s/z, l/r na th/dh)<br>e) kuchangamkia kukariri vitanzandimi vinavyotungwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi: f/v, s/z, l/r na th/dh) ili kuimarisha matamshi yake. | zinazokaribiana kimatamshi: f/v, s/z, l/r na th/dh ili kuimarisha mawasiliano,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga vitanzandimi vyenye maana kutokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi: f/v, s/z, l/r na th/dh)<br>● Mwanafunzi achangamkie kukariri vitanzandimi vinavyotungwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi: f/v, s/z, l/r na th/dh) ili kuimarisha matamshi yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana katika kutamka silabi na kuunda vitanzandimi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anakuza ujuzi wa kidijitali anapotumia vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kusikiliza sauti na kuunda vitanzandimi mtandaoni.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoendelea kukariri vitanzandimi na kusakura mtandaoni ili kupata vitanzandimi zaidi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka kwa usahihi silabi zinazotokana na sauti lengwa na kuunda vitanzandimi sahihi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anafikiria kwa kina anapounda vitanzandimi vyenye sauti lengwa.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuunda vitanzandimi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali vinavyotumika kutambua silabi za sauti lengwa kutokana na maneno. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia mtandao salama mwanafunzi anaposakura kuhusu vitanzandimi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili pia huifundisha matamshi bora. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Mgeni mwalikwa, vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, vitabu vya breli, kinasasauti, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vye breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1**<br>**Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu,<br>b) kutambua nukta nundu za nusu kistari, kistari, alama za usemi na alama za mabano mzunguko(asieona),<br>c) kutumia msamiati lengwa kwa usahihi katika sentensi,<br>d) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika,<br>e) kuonyesha uelewa wa kifungu kwa kutoa muhtasari na kujibu maswali, | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua msamiati wa suala lengwa (k.v. *vyakula, viungo vya kupikia, njia za kupika na vifaa vya kupikia*) kwa kutumia kadi za maneno, chati, mti maneno au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua msamiati wa swala lengwa akitumia orodha maneno, kadi za breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nukta nundu za nusu kistari, kistari, alama za usemi na alama za mabano mzungiko za breli anaposoma. | 1. Kusoma kuhusu mapishi kuna umuhimu gani?<br>2. Msamiati hutumika kivipi kuongeza utamu wa hadidhi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | f) kujenga mazoea ya usomaji bora katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi ashiriki katika vikundi kujadili na kutumia msamiati wa suala lengwa katika sentensi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu kuhusu suala lengwa kwenye kitabu au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutoa muhtasari kuhusu kifungu alichosoma.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujibu maswali kutokana na kifungu alichosoma.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma vifungu mtandaoni kuhusu suala lengwa na kujadiliana na wenzake kuhusu ujumbe uliomo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi ya vikundi na kutumia msamiati wa suala lengwa katika sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anakuza ujuzi wa kidijitali anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma kifungu.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzae katika shughuli za vikundi.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu kazi za wenzake kwenye kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma vifungu vinavyoeleza kuhusu mapishi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hushughulikia vifungu vya hadithi na upanuzi wa msamiati. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Orodha maneno, kadi maneno, kadi za breli, mti maneno, kapu maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Insha ya wasifu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya wasifu kwa kuzingatia mtindo na muundo wake, | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya wasifu kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma vielelezo vya insha ya wasifu | 1. Insha ya wasifu hutofautiana na insha nyingine kivipi?<br>2. kwa nini ni muhimu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | b) kuandika insha ya wasifu kwa ubunifu ili kujenga maelezo yenye kutoa picha dhahiri,<br>c) kuandika insha ya wasifu akizingatia nukta nundu za nusu kistari, kistari, alama ya usemi na alama za mabano mzunguko (asiyeona)<br>d) kufurahia kutunga insha bora ili kuimarisha mazoea ya kuandika. | vilivyoandikwa katika matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya wasifu.<br>● Mwanafunzi akishirikiane na wenzake katika vikundi ili kubainisha na kujadili vidokezo vifaavyo vya mada lengwa.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha ya wasifu isiyopungua maneno 150 inayohusu mada lengwa (k.v. *Mpishi nimpendaye*) kwa kuzingatia, anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, kanuni za kisarufi (k.v uakifishaji mwafaka na tahajia) na kwa lugha ya kiubunifu inayojumuisha methali, tashbihi na nahau alizojifunza awali, mwanafunzi asiyeona aandike insha ya wasifu isiyopungua maneno 150 inayohusu mada lengwa (k.v. *Mpishi* | kuambunifu unapoandika insha ya wasifu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *nimpendaye*) kwa kuzingatia, anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, nukta nundu zifaazo, kanuni za kisarufi (k.v *uakifishaji mwafaka na tahajia*) na kwa lugha ya kiubunifu inayojumuisha methali, tashbihi na nahau alizojifunza awali.<br>• mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya wasifu akizingatia matumizi ya nukta nundu za breli za nusu kistari, kistari, alama za usemi na alama za mabanu.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya wasifu mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini.<br>• Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili kumpa motisha kuandika zaidi.<br>• Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake insha ya wasifu aliyoandika ili apate maoni. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya wasifu.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya wasifu. |
| **Maadili:**<br>● Heshima na adabu: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za vikundi na kuthamini maoni ya wenzake.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.<br>● Uadilifu: mwanafunzi anapoandika insha ya wasifu kuhusu watu ambao wanajulikana kwa matendo mema. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Elimu ya afya na kujikinga: mwanafunzi anapofanya kazi pamoja katika vikundi mwanafunzi anajifunza mambo ya afya. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hushughulikia uandikshi wa insha. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya wasifu, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1**<br>**Aina za Nomino:**<br><br>*Nomino za Pekee*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za pekee kwenye sentensi au vifungu vya maneno,<br>b) kutunga sentensi kwa kutumia nomino za pekee ili kukuza matumizi ya lugha sahihi,<br>c) kuchangamkia kutumia nomino za pekee katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za pekee (*k.v. Kisumu, Mei, Rabuka, Alhamisi na Yohana*) kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno au chati, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za pekee kwenye orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● *Mwanafunzi* akiwa na wenzake ataje nomino za pekee kama vile za majina ya miji, majina ya mito, majina ya watu na majina ya miezi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za pekee katika sentensi kwenye vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, tarakilishi, chati kwa kuzipigia mstari au kukolezea rangi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za pekee katika sentensi na aziandike kwenye | 1. Ni jinsi gani utatambua nomino za pekee?<br>2. Je unatambaje nominoza pekee? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | matini za breli na tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ajaze nafasi kwa kutumia nomino za pekee.<br>● *Mwanafunzi* aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia nomino za pekee akiwa peke yake, wawiliwawili au vikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua nomino za pekee.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia nomino za pekee.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino za pekee na kuzitungia sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya kazi ya vikundi.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini wenzake wakitaja nomino za pekee.

**Masuala Mtambuko:**
Mshikamano wa kijamii na utaifa: unatokea kwenye kazi za vikundi wakati mwanafunzi anashirikiana na wenzake.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English: somo hili pia linashughulikia kutambua na kutumia aina za maneno kama vile nomino.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia** |
|---|
| Kadi maneno, kadi za breli, mti maneno, kapu maneno, vifaa vya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.2**<br>**Aina za Nomino**<br>Nomino za kawaida<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za kawaida kwenye sentensi au vifungu vya maneno,<br>b) kutunga sentensi kwa kutumia nomino za kawaida ili kukuza matumizi sahihi ya lugha,<br>c) kufurahia kutumia nomino za kawaida katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za kawaida kwenye kadi au kapu la maneno *(k.v.mtu, mtoto, darasa, ukuta, mwalimu, meza na kiti)*, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za kawaida kwenye orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutaja nomino za kawaida.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za kawaida katika sentensi kwa kuzipigia mistari au kuzikolezea rangi kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za kawaida na kuziandika kwenye karatasi za | 1. Nomino za kawaida hutofautiana na nomino nyingine kivipi?<br>2. Nomino za kawaida hutumika kivipi katika sentensi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino za kawaida kujaza nafasi kwenye sentensi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia nomino za kawaida akiwa peke yake wawiliwawili au kwenye vikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi na kujaza nafasi.
- Mawasiliano na ushirikiano :mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi kutaja nomino na kutunga sentensi.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapotagamana na wenzake kwenye vikundi.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wengine kwenye kikundi.

Maadili mbalimbali yanaweza kulengwa katika sentensi k.v. upendo, uaminifu, uzalendo, amani na umoja.

**Masuala Mtambuko:**
Mshikamano wa kijamii na utaifa: mwanafunzi anapofanya kazi za vikundi wakati mwanafunzi anashirikiana na wenzake.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili linashughulikia utambuzi na matumizi ya aina za maneno kama vile nomino.

| |
|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kadi maneno, kadi za breli, mti maneno, kapu maneno, vifaa vya breli na tarakilishi yenye teknolojia saidizi. |

## 2.0 HUDUMA YA KWANZA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1**<br>**Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1**<br>**Maamkuzi na Maagano**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano,<br>b) kueleza maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali ili kuyabainisha,<br>c) kutumia aina mbalimbali za maamkuzi na | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maamkuzi (*k.v. shikamoo*, *Habari za utokako? Habari za adhuhuri? Habari za jioni?)* kutoka kwenye chati, ubao au vifaa vya kidijitali, michoro na picha, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maamkuzi kutoka kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, maelezo ya picha na maelezo ya michoro. | 1. Je, watu husalimiana vipi katika jamii?<br>2. Je, ni jinsi gani watu huagana katika jamii? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | maagano katika mawasiliano,<br>d) kuchangamkia maamkuzi na maagano katika mahusiano. | • Mwanafunzi ashiriki kujadiliana na mwenzake au katika vikundi maamkuzi yanayolengwa na matumizi yake.<br>• Mwanafunzi Aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maagano (*k.v lala salama, safari njema, alamsiki)* kutoka kwenye chati, ubao au vifaa vya kidijitali, michoro na picha, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maagano kutoka kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, maelezo ya picha na maelezo ya michoro.<br>• Mwanafunzi ashirikiana na wenzake kuigiza maamkuzi na maagano lengwa.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu atazame watu wakiamkuana na kuagana katika vifaa vya kidijitali | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vyenye kidijitali, mwanafunzi asiyeona asikilize watu wakiamkuana na kuagana katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aambatanishe maamkuzi na maagano na majibu sahihi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza maamkuzi na maagano.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kujifunzia.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia maamkuzi na maagano ipasavyo.

**Maadili:**

- Heshima: aamkuzi huimarisha heshima.
- Upendo: Maamkuzi huashiria upendo.
- Umoja: Maamkuzi huimarisha umoja na uhusiano mwema.

**Masuala Mtambuko:**
Utangamano wa kijamii: Mwanafunzi anapoamkuana na kuagana na wenzake.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: Somo hili hushughulikia maamkuzi na maagano.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Maelezo ya picha, maelezo ya michoro na vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli.

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **kusoma** | **2.2.1**<br><br>**Kusoma kwa Kina**<br><br>*Matumizi ya Kamusi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mpangilio wa maneno katika kamusi *au mtandaoni* ili kupata maneno lengwa kwa urahisi,<br>b) kutaja alama za nusu kistari, kistari, alama za usemi na alama za mabano mzunguko(asieona),<br>c) kutumia kamusi *au mtandao* ipasavyo kutafuta maana za maneno asiyoyajua yaliyo katika matini teule ili kukuza msamiati wake,<br>d) kuchangamkia kutumia kamusi au mtandao katika kukuza msamiati wake. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kupanga maneno aliyopewa kwenye chati, kapu maneno au mti maneno kialfabeti, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kupanga maneno aliyopewa kwenye orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kialfabeti.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua neno kutoka kapu maneno au mti maneno ili kulitafuta kwenye kamusi mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua neno kutoka orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi na kulitafuta mtandaoni. | Kwa nini tunatumia kamusi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kutumia kamusi au mtandao kutafuta maana za maneno mbalimbali akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutafuta maana za maneno.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia mtandao kutafuta maana za maneno.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia kamusi kutafuta maana ya maneno.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoanza kutumia kamusi kutafuta maana za maneno.

**Maadili:**

- Uzalendo: mwanafunzi anapoweza kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa.
- Uadilifu: mwanafunzi anapotumia msamiati ufaao katika mawasiliano.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kupata maneno kwenye kamusi au mtandao.

**Masuala Mtambuko:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitegemea katika kutumia kamusi.
- Kujithamini: mwanafunzi anapofanya kazi na wengine katika vikundi.
- Masuala ya afya: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu huduma ya kwanza.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili husisitiza matumizi mbalimbali ya kamusi.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kamusi, kapu maneno, kadi za breli, chati, orodha maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1: Insha ya masimulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya masimulizi kwa kuzingatia ujumbe, mtindo na muundo,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuandika insha ya masimulizi akitumia mikato inayoundwa na nukta nundu 4,6 au 5,6 ikifuatwa na herufi.<br>d) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ya masimulizi ili kukuza ubunifu wake. | • Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha isiyopungua maneno 150 inayosimulia kisa cha tukio linalohusiana na huduma ya kwanza kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu. | Ni kwa nini insha ya masimulizi ni muhimu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • mwanafunzi aelekezwe kuandika insha isiyopungua maneno 150 akitumia nukta nundu za nusu kistari, kistari, alama ya usemi na alama za mabano mzunguko za breli(asieona).<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya masimulizi mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini.<br>• Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: wakati mwanafunzi anatumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya masimulizi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

**Maadili:**

- Heshima na adabu hasa: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za vikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za vikundi.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii na utaifa: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka jamii tofauti kufanya kazi pamoja.<br>● Masuala ya afya: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu huduma ya kwanza. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili linashughulikia uandishi wa insha mbalimbali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya masimulizi, vifaa vya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Aina za Nomino:** Nomino za Wingi<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za wingi katika matini ili kuzibainisha,<br>b) kutumia nomino za wingi katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano, | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za wingi (*k.m chumvi, sukari, maji, uji, mafuta na manukato*) kutoka kwenye kapu la maneno, chati, vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza na vifaa vya kidijitali akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za wingi kutoka kwenye | Ni muhimu kutambua nomino za wingi, kwa nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | c) kufurahia kutumia nomino za wingi katika mawasiliano. | orodha maneno, vitabu vya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za wingi kwa kuzipigia mistari au kuzikolezea rangi kwenye matini, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za wingi na kuziandika kwenye karatasi za breli.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino za wingi kujaza nafasi kwenye sentensi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia nomino za wingi katika sentensi kwa kufanya mazoezi daftarini, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia nomino za wingi katika sentensi kwa kufanya mazoezi kwenye karatasi za breli. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Kufikiri kwa kina: mwanafunzi anapotunga sentensi na kuzijadili na wenzake.

| |
|---|
| • Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua nomino za wingi. |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhiriki kwenye vikundi.<br>• Uwajibikaji: Mwanafunzi anawajibika kukamilisha kazi zake pamoja na kutunza vifaa vya kidijitali kama vile tarakalishi. |
| Masuala Mtambuko:<br>• Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwenye kikundi.<br>• Kujithamini: mwanafunzi anapokuza stadi ya kujieleza kupitia utungaji wa sentensi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili pia linafunza kuhusu nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kapu maneno, chati, tarakilishi yenye teknolojia saidizi,vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.2**<br>**Aina za Nomino:**<br>*vitenzi-jina*<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za vitenzi-jina kwenye kifungu cha maneno au kwenye sentensi,<br>b) kutunga sentensi au vifungu vya maneno akitumia nomino za vitenzi-jina ili kukuza matumizi bora ya lugha,<br>c) kufurahia kutumia nomino za vitenzi- jina katika utungaji wa sentensi na kujaza nafasi.. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za vitenzi-jina kutoka kwenye kapu la maneno, vyombo vya kijiditali vyenye teknolojia saidizi (*k.v. kusoma*, *kucheka*, *kula*, *kulia na kuandika*.) mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za vitenzi-jina kutoka kwenye orodha maneno, kadi za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe atambue nomino za vitenzi-jina akiwa na wenzake kwa kuvipigia mistari au kuzikolezea rangi kwenye matini, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua na kuandika nomino lengwa kwenye karatasi za breli. | 1. Nomino za vitenzi jina hutumika vipi?<br>2. Jinsi gani vitenzi jana hutumika kuonyesha vitendo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino za vitenzi-jina kwa kujaza nafasi kwenye sentensi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi au vifungu vya maneno kwa kutumia nomino za vitenzi-jina akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotunga sentensi na kuzijadili na wenzake.
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine kwenye kazi za kikundi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowatungia wenzake sentensi katika makundi.

**Maadili:**

- Upendo: mtakuzwa mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwenye vikundi kufanya shughuli mbalimbali.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anawajibika kukamilisha kazi zake pamoja na kutunza vifaa vya kiteknolojia kama vile projekta na tarakalishi.

**Masuala Mtambuko:**

- Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwenye kikundi.
- Utaifa: mwanafunzi anapotagusana na wenzake wenye asili tofauti kwenye kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English: somo hili pia linafunza kuhusu nomino.

| |
|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kapu maneno, orodha maneno, kadi za breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

**3.0 MAPAMBO**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya UjifunzajiYanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Vitendawili**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitendawili vya suala lengwa,<br>b) kutega na kutegua vitendawili ili kujenga matamshi bora,<br>c) kuchangamkia matumizi ya vitendawili kama njia ya kujenga utamkaji bora wa maneno. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vitendawili vya mapambo katika chati, ubao au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (*k.m Wafaa lakini wavaliwa bila matumizi maalum (Mtandio), Ananitazama, hasemi hasikii (Picha), Lapendeza rangi lakini halidumu (Ua). Dhahabu yangu ya thamani haisimami (Mkufu]*, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vitendawili vya mapambo katika orodha ya vitendawili au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (*k.m Wafaa lakini wavaliwa bila matumizi maalum (Mtandio), Ananitazama, hasemi hasikii* | Je, kwa nini ni muhimu kutega na kutegua vitendawili? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>(Picha), Lapendeza rangi lakini halidumu (Ua). Dhahabu yangu ya thamani haisimami (Mkufu],<br>● Mwanafunzi ashiriki katika kutega na kutegua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana wakiwa wawiliwawili au katika vikundi,<br>● Mwanafunzi asikilize vitendawili vikitegwa na kuteguliwa kupitia vyombo vya kidijitali.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anashiriki katika kutega na kutegua vitendawili kwenye vikundi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofikiria kuhusu majibu ya vitendawili.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikiliza vitendawili vikitegwa na kuteguliwa.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutega na kutegua vitendawili.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>● Heshima: mwanafunzi anachangamkia maoni ya wenzake.<br>● Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi katika vikundi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala Mtambuko:<br>● Umoja wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika vikundi.<br>● Kujithamini: mwanafunzi anapotega na kutegua vitendawili.</td></tr>
</table>

| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: Somo hili hushughulikia vitendawili. |
|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Chati, ubao, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, orodha ya vitendawili, vifaa vya breli, vifaa halisi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1**<br>**Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha,<br>b) kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu kwa kasi ifaayo,<br>d) kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo,<br>e) kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji | ● Mwanafunzi aelekezwe kujadiliana na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame vielelezo vya video vinavyoonyesha usomaji fasaha wa makala (*k.v. hotuba*, *habari*,) na wenzake, mwanafunzi asiyeona asikilize vielelezo vya video vinavyozungumzia usomaji fasaha wa makala (*k.v. hotuba*, *habari*,) na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha habari kwa kuzingatia matamshi bora.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha habari kwa kasi isiyopungua maneno 80 kwa dakika moja kuhusu suala lengwa. | Kwa nini ni muhimu kusoma kuhusu mapambo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu akizingatia sauti ifaayo (k.v. kiwango cha sauti na kiimbo).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo panapofaa (k.v. ishara za uso na mikono zinazozingatia tamaduni).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na mzazi au mlezi kusoma makala akizingatia vipengele vya usomaji bora. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotunga sentensi akiwa na wenzake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojibu maswali kutokana na kifungu cha hadithi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kutafuta msamiati wa mapambo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza sentensi zilizotungwa na wenzake.
- Upendo: mwanafunzi anaposoma hadithi akisaidiana na wenzake.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.

**Masuala Mtambuko:**

Kujithamini: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu shughuli za vikundi na kuzikamilisha.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English: somo hili linashughulikia pia kusoma kwa ufasaha.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia** |
|---|
| Vifaa halisi, picha za mapambo, maelezo ya picha za mapambo, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1**<br><br>**Kuandika kwa Tarakilishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sehemu mbalimbali za tarakilishi zinazotumika kupigia chapa,<br>b) kutumia tarakilishi ili kujenga maarifa ya kidijitali,<br>c) kujenga mazoea ya kutumia tarakilishi kuandika na kuhifadhi maandishi. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua sehemu mbalimbali za tarakilishi za kupigia chapa. (*k.v. bodidota, kipanya na kiwambo/ mulishi*), mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua sehemu mbalimbali za tarakilishi za kupigia chapa kwa kupapasa. (*k.v. bodidota, kipanya na kiwambo/ mulishi*).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kuandika maneno au sentensi zinazolenga msamiati wa mapambo (k.v. *herini, vipuli, pete, kipini, bangili, shanga, taji, kugesi* na *hina).*<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi | Ni kwa nini tarakilishi ni kifaa cha muhimu kwetu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuandika kifungu kinachohusisha mapambo mbalimbali.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuhifadhi kazi yake kwenye faili ya tarakilishi mara kwa mara.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuhariri kazi yake kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutuma kazi yake kwa mwalimu ili kuitathmini.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kufanya mazoezi ya kuandika kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi akisaidiwa na mzazi/mlezi wake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika na kuhifadhi kazi yake.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotagusana na vyombo vya kidijitali kama vile kutumia kipakatalishi, rununu.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anapohariri kazi yake kwenye tarakilishi akishirikiana na wenzake katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapohifadhi vyombo vya kidijitali anavyotumia.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya maendeleo endelevu: mwanafunzi anapotumia ujuzi wa kidijitali ya kisasa kufanikisha uandishi.

| **Uhusiano wa Masomo Mengine**<br>English: somo hili linahimiza matumizi ya vyombo vya kidijitali. | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa halisi, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi,vifaa vya breli | | | | |
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1**<br>**Aina za Nomino**<br><br>*Nomino za Makundi*<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za makundi katika matini ili kuzibainisha,<br>b) kutumia nomino za makundi katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia nomino za makundi katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za makundi *(k. v mlolongo wa magari, tita la kuni, mkungu wa ndizi, safu ya siafu, koja la maua, bunda la noti)* katika chati, kadi maneno, ubao, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za makundi *(k. v mlolongo wa magari, tita la kuni, mkungu wa ndizi, safu ya siafu, koja la maua, bunda la noti)* katika orodha maneno na vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. | 1. Nomino za makundi hutofautiana na nomino nyingine kivipi?<br>2. Je, nomino za makundi hutumiwa vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia nomino za makundi katika sentensi na kuziandika daftarini mwake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia nomino za makundi katika sentensi na kuziandika kwenye karatasi za breli.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino za makundi kutunga sentensi mtandaoni akiwa na wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anashiriki katika majadiliano ya nomino za makundi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojibu swali dadisi lililopendekezwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutunga sentensi mtandaoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia nomino za makundi.
- Uwazaji wa kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapofanya kazi na kuthamini maoni ya wenzake katika vikundi.
- Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi katika vikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapokamilisha kazi yake kwa wakati ufaao.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Utaifa: Mwanafunzi anaposhiriki katika vikundi vinavyojumuisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali.<br>● Utangamano wa kijamii: Mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za vikundi na kujifunza ukakamavu na kujiamini. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hushughulikia dhana ya nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa vya breli, chati, kadi maneno, kadi za breli, orodha maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.2**<br>**Aina za Nomino**<br><br>*Nomino Ambata*<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino ambata katika matini ili kuzitofautisha na aina nyingine za nomino,<br>b) kutumia nomino ambata kwa usahihi katika sentensi ili | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino ambata (*k.v askarikanzu, mbwamwitu, mwanasiasa na mwananchi*) kwa kutumia kadi maneno, kapu maneno, chati au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au katika kikundi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino ambata (*k.v askarikanzu, mbwamwitu, mwanasiasa na mwananchi*) kwenye orodha maneno kadi za breli au kwenye | Kwa nini tunaunganisha nomino kuunda neno? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuimarisha mawasiliano,<br>c) kuonea fahari matumizi ya nomino ambata katika mawasiliano. | vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au katika kikundi.<br><br>● Mwanafunzi ajadili katika kikundi au wawiliwawili maana ya nomino ambata huko akitoa mifano,<br><br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia nomino ambata katika sentensi na kuziandika katika daftari lake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia nomino ambata katika sentensi na kuziandika kwenye karatasi za breli.<br><br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino ambata kutunga sentensi mtandaoni akishirikiana na wenzake.<br><br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusakura mtandaoni ili kupata mifano zaidi ya nomino ambata na kuziandika katika daftari lake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusakura mtandaoni ili kupata mifano zaidi ya nomino ambata na kuziandika katika karatasi za breli. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano ya nomino ambata.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata mifano ya nomino ambata.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutunga sentensi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia nomino ambata kwa usahihi.

**Maadili:**

- Heshima: wanafunzi wanapofanya kazi kwa zamu.
- Umoja: wanafunzi wanapofanya kazi pamoja katika vikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapokamilisha kazi yake.

**Masuala Mtambuko:**

Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za vikundi na kujifunza ukakamavu na kujiamini.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English: somo hili hushughulikia dhana ya nomino ambata.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Vifaa vya breli, chati, kadi maneno, kadi za breli, orodha maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.3 Aina za Nomino**<br>*Nomino za dhahania*<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za dhahania katika matini mbalimbali,<br>b) kuelezea nomino za dhahania kwa kutoa mifano mwafaka,<br>c) kutumia nomino za dhahania kwa usahihi katika sentensi,<br>d) kuonea fahari matumizi ya nomino za dhahania katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino za dhahania (*k.v upendo*, *uhodari*, *ukweli*) kwa kutumia kadi maneno, mti maneno, chati au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino za dhahania (*k.v upendo*, *uhodari*, *ukweli*) kwa kutumia orodha maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ajadili katika kikundi au wawiliwawili maana ya nomino za dhahania huko akitoa mifano.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia nomino za dhahania katika sentensi na kuziandika sentensi hizo daftarini mwake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia nomino za dhahania katika sentensi na kuziandika | Ni jinsi gani nomino za dhahania hutambulika? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sentensi hizo kwenye karatasi za breli.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino za dhahania kutunga sentensi mtandaoni akishirikiana na wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano ya nomino za dhahania.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojadili katika kikundi maana ya nomino za dhahania na kutoa mifano.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutunga sentensi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia nomino za dhahania kutunga sentensi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapofanya kazi kwa zamu.
- Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi katika vikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapokamilisha kazi yake.

**Masuala Mtambuko:**

- Utaifa: mwanafunzi anaposhiriki katika vikundi vinavyojumuisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali.
- Kujithamini: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za vikundi. Katika vikundi hivyo atajifunza ukakamavu, stahamala na kujiamini.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili hufunza dhana ya nomino.

| |
|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa vya breli, chati, kadi maneno, orodha maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.4 Uakifishaji**<br>● *Herufi kubwa*<br>● *Koma*<br>● *Kikomo*<br>● *Kiulizi*<br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nukta nundu zifaazo za alama ya koma, kikomo, kiulizi katika breli(mwanafunzi asiyeona),<br>b) kutambua herufi kubwa, alama ya koma, kikomo na kiulizi katika maandishi,<br>c) kutumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi ifaavyo katika maaandishi,<br>d) kufurahia matumizi ya herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi katika maandishi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi katika maandishi.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika vikundi kuakifisha sentensi akitumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi (baadhi ya sentensi ziangazie suala lengwa).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika sentensi akitumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi ifaavyo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika sentensi zenye herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi akitumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi. | Kwa nini alama za kuakifisha hutumiwa katika maandishi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki mijadala kuhusu alama za uakifishi.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoandika sentensi akitumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi ifaavyo.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika sentensi zenye herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi akitumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi. |
| **Maadili:**<br>Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika vikundi kuakifisha sentensi akitumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotunga sentensi zinazolenga mapambo yanayotumiwa na watu tofauti tofauti na dhamani yake.<br>● Utunzaji wa mazingira: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu mazingira kwa kutumia alama lengwa uakifishaji. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hushughulikia kufunza alama mbalimbali za uakifishi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Chati, kadi za breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

**4.0 SAA NA MAJIRA**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli ya Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1**<br>Maneno ya Heshima na Adabu *(maneno yanayohusiana na udugu)*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima yanayohusiana na udugu yanayotumiwa katika mawasiliano,<br>b) kutumia maneno ya heshima yanayohusiana na udugu kwa usahihi katika mazungumzo yake ya kila siku,<br>c) kuthamini matumizi ya maneno ya heshima katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maneno ya udugu (*k.v. bwana, bibi, ndugu, binti, mama, mama mkubwa/mdogo, mjomba)* kwenye ubao, mti maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi au kapu maneno, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maneno ya udugu kwenye orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya maneno lengwa kama yanavyotumiwa katika mahusiano ya kila siku kati ya watu.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia maneno lengwa kwa usahihi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame maigizo ya watu wakitumia maneno ya udugu kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na video, | Je, tunatumia maneno ya heshima na adabu kwa nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mwanafunzi asiyeona asikilize maigizo ya watu wakitumia maneno ya udugu kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ajadili matumizi ya maneno ya udugu akishirikiana na wenzake darasani.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza mazungumzo mafupi akiwa na wenzake huku akitumia msamiati wa udugu. | |

**Utmilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ujuzi wa kidijitali:  mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi, video na projekta kutazama au kusikiliza maigizo mafupi.
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika maigizo na mijadala.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapotumia maneno ya udugu.
- Upendo: mwanafunzi anapotumia maneno ya udugu kwa wenzake na kwa wakubwa wake.

**Masuala Mtambuko:**

- Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika maigizo mafupi.
- Haki za kijamii: mwanafunzi anapotumia maneno ya udugu katika mawasiliano.

| |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>English na Religious Studies: lugha ya heshima na adabu hufunzwa katika masomo haya. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Mti maneno, kapu maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli ya Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1**<br>**Kusoma kwa Mapana**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali,<br>b) kutambua msamiati wa suala lengwa katika matini ya kidijitali,<br>c) kusakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma vyenye suala lengwa,<br>d) kuchangamkia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma | • Mwanafunzi azingatie hatua za kiusalama katika kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi k.v. kufungua mitandao ifaayo.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutambua mitandao salama yenye matini inayohusu suala lengwa (saa na majira) na inayoafiki kiwango chake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutambua umuhimu wa kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi wake endapo atapata ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni na kutowasiliana nao. | Je, kwa nini tunasoma matini ya kidijitali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ujumbe ili kuimarisha maarifa yake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kusoma matini kwa kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi yanayojumuisha msamiati wa saa *(k.v. kasoro dakika…, saa… kamili, saa…na dakika…)* na majira (nyakati za siku) (*k.v. alfajiri, asubuhi, adhuhuri, alasiri, thenashara, machweo na macheo*).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma vifungu vyenye suala lengwa ambavyo alisakura.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutoa habari kuhusu matini aliyosoma kwa muhtasari na kujibu maswali katika maandishi au mazungumzo na wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusakura na kusoma matini.
- Hamu ya kujifunza: mwanafunzi atapata hamu ya kutafuta matini za kusoma kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na mitandaoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposakura vifungu vyenye suala lengwa na kuwatolea wenzake habari za matini yenyewe.
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasiliana na wenzake kutoa habari kuhusu matini aliyosoma kwa muhtasari.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza wa vifaa vya kidijitali na kuzingatia mitandao salama.
- Uadilifu: mwanafunzi anapohakikisha anasakura matini kwenye tovuti salama.
- Heshima: mwanafunzi anapowasiliana na mwalimu,mzazi au mlezi.

**Masuala Mtambuko:**

- Usalama: mwanafunzi anapozingatia hatua za kiusalama mtandaoni.
- Utunzi wa usalama wa watoto**:** mwanafunzi anapotangamana na wenzake wakitumia vifaa vya kidijitali.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
Masomo yote kwa vile yanatakiwa kuzingatia ujuzi wa kidijitali.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Projekta, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1: Baruapepe**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua baruapepe kwa kuzingatia muundo wake,<br>b) kuandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo,<br>c) kuchangamkia uandishi wa baruapepe katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua muundo wa baruapepe kwa kurejelea kielelezo chake kilichochapishwa au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ajadili sehemu mbalimbali za baruapepe kama vile anwanipepe ya mtumaji (k.m. tina18@gmail.com), anwanipepe ya mpokeaji, mada ya baruapepe, mtajo, mwili, hitimisho na jina la mwandishi/ mtumaji.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika baruapepe kwa rafiki, ndugu, au mzazi akishirikiana na wenzake darasani, kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi akizingatia muundo wa uandishi wa baruapepe, utaratibu ufaao, kutunga na kupanga sentensi kuunda aya katika uandishi wa baruapepe.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili mada ya baruapepe na vipengele vyake vinavyofaa kujumuishwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuaandika baruapepe kwa rafiki kwa kuzingatia ubora wa sentensi (sahihi kisarufi, zilizokamilika kimaana, zenye kufuatana kwa kujenga | 1. Je, tunaandika barua pepe kwa nini?<br>2. Je, tunaandika barua pepe vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wazo na zenye kuzingatia uakifishi mzuri) kuunda aya.<br>● Mwanafunzi ashirikishe msamiati wa mada lengwa katika baruapepe yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika baruapepe na kuituma kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na kujadiliana na wenzake kuhusu baruapepe.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika na kutuma baruapepe.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kuandika na kutuma baruapepe.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoandika baruapepe na kuwapa wenzake waitathmini.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapotuma baruapepe kwa rafiki, mzazi au mlezi wake kuwajulia hali.
- Heshima: wanafunzi anapozingatia maoni ya wengine wakati wa mijadala.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza tarakilishi anayoitumia katika uandishi wa baruapepe.

**Masuala Mtambuko:**

- Kujithamini: mwanafunzi anapotumia baruapepe kuwasiliana.
- Elimu kwa maendeleo endelevu: mwanafunzi anapotumia teknolojia kuwasiliana.
- Elimu ya mazingira: mwanafunzi anapoandika sentensi sahihi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
Masomo yote yanayoshughulikia ujuzi wa kidijitali

| |
|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha barupepe, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli ya Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Ngeli I-ZI**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-ZI katika sentensi,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya I-ZI ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi,<br>d) kuonea fahari matumizi ya nomino katika ngeli ya I-ZI katika mawasiliano. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua viambishi vya ngeli ya I-ZI katika sentensi kwa kuvipigia mstari daftarini au kuvikoleza rangi katika tarakilishi, mwanunzi asiyeona aelekezwe kutambua viambishi vya ngeli ya I-ZI katika sentensi kwa kuviorodheresha kwenye karatasi za breli.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya I-ZI kwenye kadi, mti maneno, tarakilishi au kapu la maneno *(k.v. nguo- nguo, ndizi- ndizi, ndoo-ndoo na nyumba-nyumba*), mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya I-ZI kwenye kadi za breli, orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi *(k.v. nguo-nguo, ndizi- ndizi, ndoo-ndoo na nyumba-nyumba*). | Je, nomino katika ngeli ya I-Z hutambulika vipi? |

<table>
<tr>
<td></td>
<td></td>
<td></td>
<td>
<ul>
<li>Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino za ngeli ya I-ZI katika sentensi akiwa peke yake au katika vikundi.</li>
<li>Mwanafunzi asikilize usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya I-ZI kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti.</li>
<li>Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya I-ZI akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake</li>
<li>Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi kwa kutumia viambishi vya nomino za ngeli ya I-ZI.</li>
</ul>
</td>
<td></td>
</tr>
<tr>
<td colspan="5">
Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa
<ul>
<li>Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia nomino za ngeli ya I-ZI katika sentensi akiwa katika vikundi.</li>
<li>Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kwa kutumia nomino za ngeli ya I-ZI.</li>
<li>Uwazaji wa kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu sentensi sahihi katika ngeli ya I-ZI.</li>
<li>Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kutambua viambishi vya ngeli ya I-ZI katika sentensi.</li>
</ul>
</td>
</tr>
<tr>
<td colspan="5">
Maadili:
<ul>
<li>Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya kazi yake kikamilifua kama vile kujaza nafasi kwa kutumia viambishi vya nomino za ngeli ya I-ZI.</li>
<li>Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi na wengine kwenye vikundi.</li>
<li>Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi.</li>
</ul>
</td>
</tr>
</table>

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapofanyafanya kazi kwa vikundi.<br>• Kujithamini: mwanafunzi anapojifanyia kazi darasani. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: Somo hili linafunza ngeli mbalimbali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kadi maneno,kadi za breli, mti maneno, orodha maneno,tepurekoda, kinasasauti, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

## 5.0 KUKABILIANA NA UMASKINI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Methali:** *Methali zinazohusu bidii* <br><br> (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze: <br> a) kutambua methali zinazohusu bidii ili kuzitofautisha na aina zingine za methali, <br> b) kueleza maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu bidii katika jamii, <br> c) kutumia methali zinazohusu bidii katika mawasiliano, <br> d) kuchangamkia matumizi ya methali katika kuhimiza bidii. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua methali zinazohusu bidii (*k.v. mchagua jembe si mkulima, mgagaa na upwa hali wali mkavu, atafutaye hupata, anayejitahidi hufaidi, ukiona vyaelea vimeundwa*) katika chati, ubao, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua methali zinazohusu bidii (*k.v. mchagua jembe si mkulima, mgagaa na upwa hali wali mkavu, atafutaye hupata, anayejitahidi hufaidi, ukiona vyaelea vimeundwa*) katika orodha ya methali, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. <br> ● Mwanafunzi ajadili maana na matumizi ya methali zinazohusu bidii na wenzake darasani. <br> ● Mwanafunzi atoe mifano ya methali zinazohusu bidii. | Je, methali hutumiwaje katika jamii? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi asikilize methali zinazohusu bidii zikitumiwa kupitia vyombo vya kidijitali.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wenzake katika kukamilisha methali zinazohusu bidii.<br>• Mwanafunzi asakure mtandaoni kwa kusaidiwa na mzazi au mlezi wake ili kupata methali zaidi zinazohusu bidii na matumizi ya methali hizo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kujadili methali kwenye vikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofikiria kuhusu matumizi ya methali.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotumia methali kujieleza.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolijia saidizi kutambua methali na kupata methali zaidi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kukamilisha methali zinazohusu bidii.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposakura methali mtandaoni salama.

**Masuala Mtambuko:**

- Umaskini: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu umaskini.
- Elimu ya fedha: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake methali zinazohusu bidii.

| |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili pia hushughulikia dhana ya methali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Chati, orodha ya methali, ubao, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu:**<br>*Ushairi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mizani na vina katika shairi ili kuvibainisha,<br>b) kusoma shairi akizingatia vina, mizani na ujumbe ili kuimarisha ufahamu,<br>c) kuchangamka kusoma shairi akizingatia mapigo ya sauti. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vina na mizani katika shairi lililochapisha au la mtandaoni.<br>● mwanafunzi ajadili vina na mizani katika shairi akiwa na mwenzake au katika kikundi,<br>● Mwannafunzi ashirikiane na mwenzake kusoma shairi akizingatia vina, mizani na ujumbe,<br>● Mwanafunzi asikilize shairi likisomwa kwa mahadhi kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au na mgeni mwalikwa na kujadili vina, mizani na ujumbe wake. | Je, mashairi hutumika vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kutafuta mashairi mtandaoni na kujadili vina, mizani na ujumbe uliomo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kujadili msamiati unaotumika katika shairi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojadili ujumbe katika shairi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofafanua ujumbe wa shairi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutambua vina na mizani katika shairi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu ushairi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutafuta mashairi mtandaoni na kujadili vina, mizani na ujumbe uliomo

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Ushauri nasaha: mwanafunzi anapozingatia ujumbe katika shairi.<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi ya vikundi na wenzake kutoka jamii mbalimbali.<br>● Mawasiliano faafu: mwanafunzi anapotumia lugha kwa ufundi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hushughulikia ufuzaji wa mashairi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Mgeni mwalikwa, nakala ya shairi,vifaa vya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1**<br>**Insha ya Maelezo**<br>● *Mada*<br>● *Muundo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha za maelezo katika matini mbalimbali,<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ili kuimarisha uandishi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake kuhusu mambo muhimu yanayojenga mpangilio mzuri wa mawazo katika insha,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo (*k.v. Jinsi ninavyoweza kuchangia kukabiliana na umaskini nyumbani, Maskini alivyogeuka kuwa tajiri, Jinsi elimu ilivyosaidia kumaliza umaskini, jinsi matumizi* | Je, insha ya maelezo huandikwa vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *bora ya pesa yanavyosaidia kumaliza umaskini, jinsi ulipaji ushuru unavyosaidia kukabiliana na umaskini*) isiyopungua maneno **150** kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu unaojumuisha methali na nahau alizojifunza awali.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini,<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuitolea maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo.

- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoyatafakari Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapojadili kuhusu insha ya maelezo.
- Upendo: Mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili kuitolea maoni

**Masuala Mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapofanya kazi na wenzake kutoka jamii mbalimbali.
- Elimu ya pesa: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu jinsi ya kukabiliana na umaskini.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
English: somo hili pia hushughulikia dhana ya uandishi wa ya maelezo.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Kielelezo cha insha ya maelezo, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1**<br>**Ngeli ya U-ZI**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-ZI katika sentensi,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya U-ZI ili kuzibainisha,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya U-ZI katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi,<br>d) kufurahia matumizi ya nomino za ngeli ya U-ZI katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua viambishi vya ngeli ya U-ZI katika sentensi kwa kuvipigia mstari daftarini mwake au kuvikoleza rangi katika tarakilishi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua viambishi vya ngeli ya U-ZI katika sentensi kwa na kuviorodhesha kwenye karatasi za breli au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya U-ZI kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno *(k.m. uzi- nyuzi, ukuta-kuta, uta- nyuta, ubavu- mbavu, wakati-nyakati, ukucha-kucha na ufunguo-funguo, wimbo-nyimbo),* mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya U-ZI kwenye kadi za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi *(k.m. uzi- nyuzi, ukuta-kuta, uta-nyuta, ubavu- mbavu, wakati-nyakati, ukucha-kucha na ufunguo-* | Je, nomino katika ngeli ya U-ZI hutambulika vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *funguo, wimbo-nyimbo).*<br>• Mwanafunzi asikilize usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya U-ZI kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya U-ZI akiwa peke yake tau kwa kushirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi kwa kutumia viambishi vya ngeli ya U-ZI kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya U-ZI.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya U-ZI.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotambua viambishi vya ngeli ya U-ZI katika sentensi na kuvikoleza rangi katika tarakilishi.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vipakatalishi anavyotumia.
- Uzalendo: mwanafunzi anapofanya kazi na wengine kwenye vikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tepurekoda au kinasasauti kusikiliza usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya U-ZI.

| |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili linashugulikia pia ngeli za nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kadi,kadi za breli, mti wa maneno, vifaa vya kidjitali vyenye teknolojia saidizi, tepurekoda, kinasasauti |

**6.0 MAADILI**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Ushairi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kukariri shairi kwa kuzingatia matamshi na mahadhi mbalimbali,<br>b) kueleza maana ya msamiati uliotumiwa katika shairi,<br>c) kutumia msamiati uliotumiwa katika shairi kuboresha mawasiliano,<br>d) kuonyesha ufahamu wa ujumbe katika shairi kwa kujibu maswali,<br>e) kuchangamkia ushairi kama njia ya kujieleza kwa ufasaha. | ● Mwanafunz i aelekezwe kukariri shairi kuhusu mada lengwa (maadili) kwa kuzingatia matamshi na mahadhi mbalimbali.<br>● Mwanafunzi asikilize shairi lengwa likikaririwa au kuimbwa na mwalimu, mgeni mwalikwa (mghani) au kupitia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kukariri au kuimba shairi kwa mahadhi mbalimbali.<br>● *Mwanafunzi* atambue msamiati uliotumika katika ushairi kuhusu maadili (*k.m. haki*, *usawa*, *heshima na uwajibikaji*) na kuueleza akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake. | Ushairi unaweza kuboresha mazungumzo yako vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili ujumbe katika shairi.<br>• Mwanafunzi ajibu maswali yanayotokana na shairi alilosikiliza, aliloimba au kukariri. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposikiliza shairi lililorekodiwa likikaririrwa kupitia vyombo vya kidijitali.
- Kujiamini: mwanafunzi anajenga umilisi huu anapokariri shairi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika vikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotekeleza majukumu katika vikundi na kufuata mafunzo katika shairi.
- Upendo:mwanfunzi anapokariri shairi na wenzake na kujadili ujumbe katika shairi.

**Masuala Mtambuko:**
Kujithamini: mwanafunzi anapokariri shairi kwa mahadhi mbalimbali kwa kuzingatia matamshi na mahadhi mbalimbali.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- English: somo hili linashughulikia ufunzaji wa ushairi.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Nakala ya shairi, mgeni mwalikwa (mghani),vifaa vya kiditali vyenye teknolojia saidizi.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1**<br>**Kusoma kwa Mapana:**<br><br>*Makala ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) Kutambua makala ya kusoma katika maktaba ili kuimarisha uchaguzi bora wa Makala,<br>b) kusoma makala mbalimbali ili kujenga ufasaha wa lugha,<br>c) kufurahia kusoma makala mbalimbali ili kujenga ufasaha wa lugha. | ● Mwanafunzi aelekezwe kuchagua makala atakayosoma katika maktaba.<br>● Mwanafunzi asome makala ya aina mbalimbali ya kujichagulia.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake kuhusu makala aliyoyasoma na alichojifunza kutokana na makala hayo.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atumie kamusi kupata maana za msamiati uliotumika katika makala, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia mtandao.<br>● Mwanafunzi asaidiwe na mzazi au mlezi wake kupata makala zaidi na kuyasoma ili kujenga mazoea ya usomaji.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake kuhusu makala aliyoyasoma na alichojifunza kutokana na makala hayo, | 1. Kwa nini ni muhimu kuchagua makala ya kusoma?<br>2. Je, kwa nini kusoma makala mbalimbali ni muhimu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu makala aliyoyasoma na alichojifunza kutokana na makala hayo.<br>● Kujiamini: mwanafiunzi anposoma makala ya aina mbalimbali ya kujichagulia. |
| **Maadili:**<br>Heshima: mwanafunzi anapothamini mchango wa wenzake wakieleza waliyoyasoma na kujjifunza kutokana na Makala ya kujichagulia. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Kujithamini: mwanafunzi anaposoma makala ya aina mbalimbali ya kujichagulia.. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili huhimiza kusoma kwa mapana kama mojawapo ya stadi za lugha. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, vitabu vya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, majarida, vi, magazeti |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Kuandika Insha:**<br>**Insha za Wasifu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu,<br>b) kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia muundo na mtindo ufaao,<br>c) kufurahia uandishi wa insha za wasifu ili kukuza stadi ya kuandika. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame nakala za insha za wasifu kwenye chapa au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma nakala za insha za wasifu kwenye matini za breli na tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele muhimu vya kimuundo kama vile kichwa, mwili, hitimisho.<br>● Mwanafunzi ajadili na wenzake kuhusu kinachoweza kuandikiwa katika insha ya wasifu *(k.v. mtu, kitu, mnyama na mahali,).*<br>● Mwanafunzi ajadili na wenzake kuhusu mada mbalimbali zinazoweza kutungiwa insha za wasifu *k.m. mwanafunzi mwadilifu, mtu aliyeshinda tuzo kwa wadilifu wake* n.k. | Je, unaandikaje insha ya wasifu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha ya wasifu isiyopungua maneno **150** daftarini au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aandike kwenye karatasi za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwasomea wenzake insha aliyoiandika ili kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa**

- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotaja mada mbalimbali zinazoweza kutungiwa insha za wasifu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi katika utungaji wa insha ya wasifu
- Mawasiliano na ushirikiano**:** mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu kinachoweza kuandikiwa katika insha ya wasifu.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza kwa makini wenzake wakisoma insha zao.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapokamilisha kuandika insha ya wasifu.

**Masuala Mtambuko:**
Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: mwanafunzi anapoandika insha ya wasifu kuhusu suala lengwa katika kiwango chake.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili hushughulikia uandishi wa insha ya wasifu.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia** |
| --- |
| Kielelezo cha insha ya wasifu, matini za breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1**<br>**Ngeli ya U-YA**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-YA kwenye sentensi,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya U-YA ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya U-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi,<br>d) kufurahia matumizi ya nomino za ngeli ya U-YA katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua viambishi vya ngeli ya U-YA katika sentensi kwa kuvipigia mstari daftarini mwake au kuvikoleza rangi katika tarakilishi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua viambishi vya ngeli ya U-YA katika sentensi na kuviorodheresha kwenye karatasi za breli au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya U-YA kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno (*kama vile ubele, uovu, ugonjwa),* mwanafunzi | Je, tunabadilishaaje nomino za ngeli ya U-YA kutoka umoja hadi wingi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | asiyeona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya U-YA kwenye kadi za breli,orodha ya maneno au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi (*kama vile ubele, uovu, ugonjwa).*<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino za ngeli ya U-YA katika sentensi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi asikilize usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya U-YA kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuunda sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya U-YA akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi kwa kutumia viambishi vya ngeli ya U-YA kwa maandishi ya mkono au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi kutumia nomino za ngeli ya U-YA.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotambua viambishi vya ngeli ya U-YA katika sentensi na kuvikoleza rangi katika tarakilishi. |
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vipakatalishi anavyotumia.<br>● Uzalendo: mwanafunzi anapofanya shughuli za ujifunzaji kuhusu ngeli ya U-YA akiwa na wengine. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tepurekoda au kinasasauti kusikiliza usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya U-YA. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili linashugulikia pia ngeli za nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kadi maneno, kadi za breli, mti maneno, orodha maneno na tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

## 7.0 ELIMU YA MAZINGIRA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuliza za Ujifunzaji | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Nahau**<br><br>*Nahau za usafi na mazingira*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nahau za usafi na mazingira katika matini mbalimbali,<br>b) kufafanua maana za nahau mbalimbali za usafi na mazingira kwa kutoa mifano,<br>c) kutumia nahau za usafi na mazingira katika mawasiliano,<br>d) kuthamini matumizi ya nahau za usafi na mazingira katika mawasiliano. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nahau za usafi na mazingira (*k.v. angua kucha*, *penga kamasi*, *piga deki*, *piga mswaki*, *chokonoa meno*, *futa vumbi*) katika chati, michoro, picha, vikapu maneno, mti maneno, chati, kamusi na katika vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nahau za usafi na mazingira (*k.v. angua kucha*, *penga kamasi*, *piga deki*, *piga mswaki*, *chokonoa meno*, *futa vumbi*) katika maelezo michoro, maelezo picha na katika vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi ajadiliane na wenzake maana za nahau za | 1. Je, tunazingatia usafi vipi?<br>2. Nahau za mazingira ni muhimu, kwa nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | usafi na mazingira na kutoa mifano,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia nahau za usafi na mazingira kutunga sentensi akiwa pekee au kwa kushirikiana na wenzake.<br>● mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ashirikiane na wenzake kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia nahau mwafaka kwenye zoezi la ubaoni, vitabuni vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona ashirikiane na wenzake kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia nahau mwafaka kwenye zoezi vitabuni vya breli au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua nahau za usafi na mazingira katika matini.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake maana za nahau za usafi na mazingira na kutoa mifano.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotumia nahau ipasavyo kujieleza. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia nahau.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapojadiliana kuhusu maana za nahau za usafi na mazingira. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu nahau za usafi na mazingira.<br>● Kujithamini: mwanafunzi anapotumia nahau za usafi na mazingira katika mawasiliano. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Chati, michoro, maelezo ya michoro, picha, maelezo ya picha, vikapu maneno, mti maneno, chati, kamusi, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7.2.1**<br>**Kusoma kwa Mapana**<br>*Matini ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba,<br>b) kusoma matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa,<br>c) kufurahia usomaji wa matini za aina mbalimbali ili kujenga utamaduni wa kusoma. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua aina mbalimbali za matini *(kama vile vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, magazeti, na majarida)* kwenye maktaba, tarakilishi zenye teknolojia saidizi au kadi za katalogi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua aina mbalimbali za matini *(kama vile vitabu vya breli, magazeti, na majarida)* kwenye maktaba au tarakilishi zenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuchagua matini atakayosoma<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma matini kimyakimya ili kupata ujumbe uliopo na kufaidi matumizi ya lugha,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusimulia ujumbe kutokana na matini alizosoma kwa wenzake.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake matini alizosoma ili kuchochea hamu | 1. Kwa nini kusoma ni muhimu?<br>2. Ni vipi unavyoweza kupata matini ya kusoma?<br>3. Kusoma aina mbalimbali za matini ni muhimu, kwa nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ya usomaji wa mapana miongoni mwao. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposoma na kusimulia ujumbe aliosoma kutokana na matini za aina mbalimbali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapochagua na kusoma matini za aina mbalimbali maktabani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine na kuzingatia maoni katika mijadala.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapoazima, kutunza na kurudisha vitabu mktabani.

**Masuala Mtambuko:**

- Kujithamini: mwanafunzi anapothamini mazingira yake nay a wenzake.
- Elimu ya maendeleo endelevu: mwanafunzi anapotunza mazingira.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- Social Studies: Somo hili hufunza kuhusu utunzaji wa mazingira.
- English: Somo hili hufunza kuhusu kusoma kwa mapana.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza vilivyoidhinishwa, vitabu vya breli, magazeti, na majarida, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1**<br>**Insha ya Maelezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha za maelezo katika matini mbalimbali,<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia muundo na mtindo ufaao,<br>c) kuchangamkia utungaji wa insha za maelezo ili kuimarisha uandishi bora. | • Mwanafunzi aelekezwe kutambua vifungu vya insha za maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi (*k.v. maelezo kuhusu upandaji wa miche, kusafisha darasa, kufua nguo, kuzuia mmomonyoko wa udongo, kupanda miti)*<br>• Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha ya maelezo isiyopungua maneno **150** akizingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu unaojumuisha methali na nahau alizojifunza awali, | Je, tunaandika insha ya maelezo kivipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya maelezo isiyopungua maneno **150** akizingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, nukta nundu zifaazo, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu unaojumuisha methali na nahau alizojifunza awali,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuisikiliza na kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili kuisikiliza na kuitathmini.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima na adabu: mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake hasa katika shughuli za vikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala kuhusu muundo wa insha ya maelezo. |

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu ya mazingira: mwanafunzi anapotunga insha na kujieleza kwa kurejelea mazingira anamoishi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hushughulikia pia uandishi wa insha ya maelezo |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya maelezo, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Umoja na wingi wa nomino:** Ngeli ya KU-KU<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya KU-KU kwenye sentensi,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya KU-KU,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya KU-KU katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi,<br>kufurahia matumizi ya ngeli ya KU-KU katika mawasiliano, | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua viambishi vya ngeli ya KU-KU katika sentensi kwa kuvipigia mstari au kuvikoleza rangi katika tarakilishi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua viambishi vya ngeli ya KU-KU katika sentensi na kuviorodhesha kwenye karatasi za breli au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya KU- KU (kama vile *kupika, kufyeka, kuzuru, kukariri, kufua)* kwenye kadi, mti maneno, tarakilishi au kapu la maneno, mwanafunzi | Nomino katika ngeli ya KU-KU hutambulika kivipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | asiyeona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya KU- KU (kama vile *kupika, kufyeka, kuzuru, kukariri, kufua)* kwenye kadi za breli, orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia nomino za ngeli ya KU-KU katika sentensi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi asikilize usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya KU-KU kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya KU-KU akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake,<br>● Mwanafunzi aelekzwe | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kujaza nafasi kwa kutumia viambishi vya ngeli ya KU-KU kwa maandishi ya mkono au tarakilishi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli ya KU-KU.
- Uwazaji wa kina na utatauzi wa matatizo: mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu atakachoandika.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotambua viambishi vya ngeli ya KU-KU katika sentensi kwa kuvikoleza rangi katika tarakilishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapojaza nafasi kwa kutumia viambishi vya ngeli ya KU-KU kwa maandishi ya mkono au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali kama vile tarakilishi anayotumia.
- Uzalendo: mwanafunzi anapofanya kazi na wengine kwenye vikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya tabianchi: mwanafunzi anapothamini mazingira yake na ya wenzake.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English: somo hili pia hushughulikia ngeli za nomino.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Kadi, kadi za breli, mti  maneno, orodha maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi ,kapu la maneno, vifaa vya breli.

**8.0 NDEGE WA PORINI**

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1**<br>**Visawe**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno,<br>b) kutumia visawe ifaavyo katika mawasiliano,<br>c) kuthamini matumizi ya visawe katika mawasiliano. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maneno matatu yenye maana sawa (*k.v. nyumbani, mastakimu, chengo: barabara, tariki, baraste: jitimai, huzuni, simanzi)* kwa kutumia kapu la maneno, kadi za maneno,<br>mti maneno, kuburura kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maneno matatu yenye maana sawa kwa kutumia orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kueleza maneno matatu | Kwa nini tunatumia visawe katika mazungumzo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | yenye maana sawa akiwa peke yake au kwa kujadiliana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuambatanisha maneno matatu yenye maana sawa katika kapu maneno, mti maneno, ubao, chati, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, kadi maneno n.k, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuambatanisha maneno matatu yenye maana sawa katika orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ahusishe visawe na vifaa halisi, picha, michoro kwenye chati, kitabu au katika vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k., mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuhusisha visawe na vifaa halisi, maelezo ya picha, maelezo ya michoro, | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | orodha maneno na vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki kujadili visawe mbalimbali katika vikundi vya wanafunzi wawiliwawili au Zaidi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia kisawe kimoja kuchukua nafasi ya kingine katika sentensi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili visawe mbalimbali akiwa na wenzake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotumia kisawe kimoja kuchukua nafasi ya kingine katika sentensi.
- Ujuzi wa kidigitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua maneno matatu yenye maana sawa kwa kubururа akitumia tarakilishi.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu mjadala kuhusu visawe akiwa na wenzake.
- Umoja: mwanafunzi anapoeleza maana ya maneno matatu yenye maana sawa akiwa na wenzake.
- Upendo: wanafunzi anapothamini mchango wa wenzake wanapojadili kuhusu visawe.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapofanya shughuli za visawe akiwa na wenzake.<br>• Kujithamini: mwanafunzi anapojieleza akitumia visawe mbalimbali. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili linafunza dhana ya visawe. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kadi, kadi za breli, mti  maneno, orodha maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi , kapu la maneno |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1**<br>**Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Mchezo wa kuigiza*<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mchezo wa kuigiza katika matini,<br>b) kusoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha,<br>c) kueleza maana ya msamiati uliotumiwa katika mchezo wa kuigiza,<br>d) kuonyesha ufahamu wa mchezo wa kuigiza kwa kujibu maswali,<br>e) kuigiza mchezo mfupi ili kukuza uwezo wa kujieleza,<br>f) kufurahia kusoma michezo na kuigiza. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya mchezo wa kuigiza akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua mchezo wa kuigiza, wahusika na maelekezo katika matini mbalimbali kama vile vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, chati na vilevile kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua na kusoma mchezo wa kuigiza wahusika kwenye matini mbalimbali za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | 1. Ni kwa nini mchezo wa kuigiza ni muhimu?<br>2. Mafunzo katika mchezo wa kuigiza hujitokeza kwa jinsi gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kusoma mchezo wa kuigiza akizingatia wahusika, maelekezo na ujumbe.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano kuhusu msamiati wa suala lengwa (ndege wa porini) uliotumiwa katika mchezo wa kuigiza (*k.v. chiriku, kasuku, tai, korongo, mwewe na kanga*).<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame mchezo mfupi wa kuigiza ukiigizwa darasani au kwenye vifaa vya kidijitali yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona asikilize mchezo wa kuigiza kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuigiza mchezo mfupi aliousoma akishirikiana na wenzake. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi ashiriki mjadala kuhusu ujumbe unaojitokeza kwenye mchezo wa kuigiza.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma mchezo wa kuigiza kwenye mtandao.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kutoa muhtasari wa mchezo aliousoma.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kuuliza na kujibu maswali ya ufahamu. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki mjadala kuhusu ujumbe unaojitokeza kwenye mchezo wa kuigiza.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kufanikisha somo.
- Uwazaji kina: mwanafunzi anapong’amua ujumbe uliomo kwenye mchezo
- Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma na kuigiza mchezo

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wanyama wa porini na kuendeleza shughuli za vikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika michezo ya kuigiza

| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu ya maendeleo endelevu: mwanafunzi anapowathamini ndege wa porini. |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hushughulika pia na usomaji na uigizaji wa michezo. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Nakala ya mchezo wa kuigiza, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1**<br>**Insha ya masimulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza sifa za insha ya masimuizi ili kuibainisha,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha isiyopungua maneno **150**, inayosimulia tukio linalohusiana na ndege wa | Je, insha ya masimulizi huandikwa vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | porini kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya masimulizi katika vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini na kumwelekeza . | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya masimulizi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha ya masimulizi na kuwasambazia wenzake na mwalimu.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi kwa kurejelea vipengele vifaavyo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na wenzake.
- Umoj: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.

| **Masuala Mtambuko:**<br>Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposimulia tukio linalohusiana na ndege wa porini. |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**:<br>English: somo hili hufunza uandishi kama mojawapo ya stadi za lugha. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya masimulizi, vifaa vya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi**:<br>● *hali ya kutendewa*<br>● *hali ya kutendeka*<br>● *hali ya kutendana*<br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitenzi katika hali ya kutendewa, kutendeka na kutendana katika matini ili kuvitofautisha,<br>b) kutumia vitenzi katika hali za kutendewa, | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vitenzi katika hali za kutendewa, kutendeka na kutendana katika chati, jedwali, kapu la maneno, mti maneno, ubao na vyombo vya kidijitali vya teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vitenzi lengwa kwenye orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | Je, vitenzi vinaweza kubadilika vipi mwishoni ili kuleta maana mbalimbali?m |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kutendeka na kutendana ipasavyo anapowasiliana,<br>c) kuchangamkia matumizi ya vitenzi katika hali ya kutendewa, kutendeka na kutendana katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kunyambua vitenzi katika hali lengwa akiwa peke yake, wakiwa wawiliwawili au katika vikundi.<br>*nzi* atumie vitenzi katika hali lengwa kwenye sentensi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ashirikiane na wenzake kujaza nafasi katika jedwali la mnyambuliko wa vitenzi kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona ashirikiane na wenzake kuandika mnyambuliko wa vitenzi kwenye karaatasi za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika sentensi upya kwa kutumia vitenzi katika hali mbalimbali. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujaza nafasi katika jedwali la mnyambuliko wa vitenzi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua vitenzi katika hali mbalimbali.
- Kujiamini: wanafunzi anapotumia vitenzi katika hali mbalimbali kuwasiliana.

| |
|---|
| • Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojaza nafasi katika jedwali la mnyambuliko wa vitenzi kwa kutumia tarakilishi. |
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaponyambua vitenzi katika hali husika akiwa katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapokamilisha shughuli za somo la myambuliko wa vitenzi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika kikundi na kufanya kazi kama anavyelekezwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili pia hushughulikia mnyambuliko wa vitenzi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kadi, kadi za breli, mti maneno, orodha maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi ,kapu la maneno,vifaa vya brli |

**9.0 MAGONJWA**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo ya Kimuktadha**<br><br>*Matumizi ya lugha rasmi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua miktadha mbalimbali kunakotumiwa lugha rasmi ili kukuza mawasiliano,<br>b) kutumia lugha katika miktadha rasmi ili kufanikisha mawasiliano,<br>c) kuchangamkia matumizi ya lugha katika miktadha rasmi. | • Mwanafunzi aelekezwe kutambua miktadha kunakotumiwa lugha rasmi (*k.v ofisini*, *hospitalini*, *mahakamani na bungeni*).<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona asikilize mazungumzo rasmi kwa kutazama maigizo kwenye vyombo vya kidijitali kama vile video, rununu, runinga, tarakilishi yenye teknolojia saidizi n.k, mwanafunzi asiyeona asikilize mazungumzo rasmi ya maigizo kwenye vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile video, rununu, runinga, tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika maigizo ya mazungumzo ya | Je, lugha rasmi hutumiwa vipi katika shughuli zetu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | miktadha rasmi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika mazungumzo rasmi nje ya darasa k.m. akiwa kwenye gwaride na majilisini.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua nidhamu ya lugha inayozingatiwa katika mazingira rasmi k.m lugha ya heshima na adabu anapowasiliana. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika maigizo ya mazungumzo ya miktadha rasmi akishirikiana na wenzake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotambua nidhamu ya lugha inayozingatiwa katika mazingira rasmi anapowasiliana.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza au kutazama mazungumzo rasmi.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali.
- Heshima: mwanafunzi anapoigiza mazungumzao rasmi kwa kutumia nidhamu ya lugha inayozingatiwa katika mazingira rasmi.

**Masuala Mtambuko:**
Magonjwa ya kuambukizwa na yasiyoambukizwa: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili linashughulikia pia ujifunzaji wa mazungumzo katika miktadha rasmi.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Video, rununu, runinga, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |
|---|

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>*Matini ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini za aina mbalimbali za kusoma na kuchagua zinazomvutia,<br>b) kusoma matini alizochagua ili kufaidika na ujumbe na lugha iliyotumiwa,<br>c) kufurahia usomaji wa aina mbalimbali za matini ili kupanua mawazo yake. | • Mwanafunzi aelekezwe kuchagua matini (*k.v. vitabu, majarida, magazeti*) zinazomvutia maktabani na mtandaoni.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma matini alizochagua ili kufaidi ujumbe uliomo.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuwatolea wenzake muhtasari wa kile alichosoma kwenye matini ili kupashana ujumbe na kuchocheana kusoma zaidi kwa ajili ya kujifurahisha. | 1. Je, kwa nini unapenda kusoma?<br>2. Unachagua vipi matini Ya kusoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi ajadiliane na wenzake matini ambayo wamesoma kwa kuzingatia ukuzaji wa msamiati. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposoma na kusimulia ujumbe aliosoma kutokana na matini za aina mbalimbali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowatolea wenzake muhtasari wa kile alichosoma kwenye matini ya kujichagulia.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadiliana kuhusu matini walizosoma.
- Uwajibikaji: Mwanafunzi anapowatolea wenzake muhtasari wa kile alichosoma

**Masuala Mtambuko:**

- Magonjwa: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa kwa mapana.
- Mawasiliano faafu: mwanafunzi anapowasiliana na wenzake kwa kuzingatia ukuzaji wa msamiati.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili linashughulikia mada ya kusoma kwa mapana.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, vitabu vya breli, majarida, magazeti, matini mbalimbali ya breli vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1**<br>**Insha za Maelezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali,<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata mtindo na muundo ufaao,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wenye ujumbe mahususi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo isiyopungua maneno **150** kwa kuzingatia msamiati unaohusu suala lengwa na kwa kuzingatia vigezo kama vile: ujumbe, tahajia, anwani, muundo, mtindo, mapambo ya lugha k.v methali, nahau, tashbihi, istiari n.k. alizojifunza awali.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa | Je, unaandika vipi insha ya maelezo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuisoma na kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya maelezo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kuisambaza.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapowasikiliza wenzake wakisoma insha waliyoandika.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kwa kuzingatia vipengele husika.

**Masuala Mtambuko:**

- Maswala ya afya: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa.

Uhusiano na Masomo Mengine
English: somo hili pia hushughulikia uandishi wa insha.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Kielelezo cha insha maelezo, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1** **Vinyume vya Vitenzi** (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze: a) kutambua vinyume vya vitenzi katika matini, b) kuunda sentensi kwa kutumia vinyume vya vitenzi, c) kuchangamkia matumizi ya vinyume vya vitenzi katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vinyume vya vitenzi *(k.m. Simama- keti, cheka-lia, enda- rudi, anika-anua n.k)* katika chati, kadi za maneno, kapu maneno, mti maneno au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vinyume vya vitenzi *(k.m. Simama- keti, cheka-lia, enda- rudi, anika-anua n.k)* katika orodha maneno au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kutafuta vinyume vya vitenzi kwa kurejelea orodha ya vitenzi aliyopewa, | Je, tunatumia vinyume vya vitenzi vipi katika matini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kutalii mazingira yake na kuunda orodha ya vinyume vya vitenzi anavyovitambua,<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia vinyume vya vitenzi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi,<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuandika upya sentensi kwa kutumia vinyume vya vitenzi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutafuta vinyume vya vitenzi kwa kurejelea orodha ya vitenzi aliyopewa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia vinyume vya vitenzi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotalii mazingira yake na kutambua vitenzi na vinyume vya vitenzi hivyo.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika upya sentensi kwa kutumia vinyume vya vitenzi.
- Heshima: mwanafunzi anapohusiana na wenzake kutafuta vinyume vua vitenzi kwenye orodha.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Elimu ya maendeleo endelevu: mwanafunzi anakuza mawazo kuhusu mazingira yake anapotambua vinyume vya vitenzi kutokana na vitendo anavyovishuhudia katika jamii yake. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hushughulikia mada ya vinyume. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Orodha maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli,chati, kapu maneno,mti maneno |

**10.0 KUDHIBITI ITIKADI ZA KIDINI NA ZA KIJAMII**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Tashbihi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tashbihi za tabia katika matini ili kuzibainisha,<br>b) kutumia tashbihi za tabia kwa usahihi katika sentensi,<br>c) kufurahia matumizi ya tashbihi za tabia katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona alekezwe kutambua tashbihi za tabia *(k.v. mjanja kama sungura, mlafi kama fisi, mwenye maneno mengi kama kasuku)* katika vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, matini, chati na vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua tashbihi za tabia kwenye matini za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aeleze maana ya tashbihi mbalimbali za tabia kwa kutoa mifano. | Je, tashbihi hutumiwa vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kukamilisha tashbihi mbalimbali za tabia akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake darasani.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia tashbihi mbalimbali za tabia.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutumia tashbihi za tabia katika sentensi akiwa peke yake au katika vikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapokamilisha tashbihi mbalimbali za tabia kwa kushirikiana na wenzake.
- Hamu ya kujifunza: mwanafunzi anapotambua kutambua tashbihi za tabia katika matini.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotambua tashbihi za tabia katika vifaa vya kidijitali chenye teknolojia saidizi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapowapa nafasi wenzake kukamilisha tashbihi za tabia.
- Uwajibikaji:mwanafunzi anapokamilisha tashibihi za tabia akiwa na wenzake.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Mawasiliano faafu: mwanafunzi anapowasiliana na wenzake akihusisha tashbihi za tabia. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili pia hushughulikia ujifunzaji wa tashbihi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Chati, vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, vitabu vya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1**<br>**Matini ya Kidijitali**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali,<br>b) kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma ili kuimarisha umilisi wake wa kutumia tarakilishi,<br>c) kusakura kwenye tovuti salama ili | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama kutoka kwenye chati au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na mitandao, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua na kuzingatia hatia za kiusalama kutoka kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | Je, utatafutaje matini ya kidijitali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kupata vifungu vya kusoma,<br>d) kutumia vyombo vya kidijitali kwa urahisi kupata matini zinazolengwa,<br>e) kuchangamkia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma ujumbe ili kuimarisha maarifa yake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua jina la faili lengwa kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na kufanya mazoezi ya kufungua na kufunga.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua mitandao salama yenye matini inayoafiki kiwango na mahitaji yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua umuhimu wa kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi wake endapo atapata ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni na kutowasiliana nao.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusimulia habari kuhusu matini aliyosoma kwa wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutafuta, kusakura kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma.

| |
|---|
| • Hamu ya kujifunza: mwanafunzi anapopata hamu ya kutafuta matini za kusoma kwenye tarakilishi na mitandaoni.<br>• Ubunifu**:** mwanafunzi anapofungua na kufunga faili lengwa kwenye tarakilishi. |
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki katika utunzaji wa vifaa vya kidijitali.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi ya kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Usalama na ulinzi, kudhibiti, kuzuia uingizaji wa silaha ndogondogo na usalama wa mtandaoni: mwanafunzi anapozingatia usalama wa mtandaoni. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Masomo yote kwa vile yanahimizwa kuzingatia matumizi ya vifaa vya kidijitali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, vitabu vya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalumu ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1**<br><br>**Insha ya Masimulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya masimulizi kwa kuzingatia muundo,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha. | • Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha ya masimulizi (*k.v. kuhusu itikadi za kidini na za kijamii*, *sherehe*, *hadithi*, *ndoto*, *ndoa za lazima n.k*) isiyopungua maneno 150 akizingatia aina mbalimbali za maneno, mnyambuliko wa vitenzi, na nyakati ili kejenga picha | Je, insha ya masimulizi huandikwa vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | dhahiri ya anachokiandikia daftarini. Pia, azingatie mada, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka, lugha ya kiubunifu, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya masimulizi kwenye karatasi za breli kwa kuzingatia kanuni zifaazo k.m alama za breli za kuakifisha k.v, koma, nukta,<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya masimulizi katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini.<br>• Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | waitathmini na kumwelekeza. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kama tarakilishi kuandika insha ya masimulizi na kuisambaza kwa wenzake.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: Mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi yaliyopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anaposoma na kutathmini insha za wenzake bila upendeleo.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika insha kwa kufuata kanuni zifaazo. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili mada na muundo wa insha ya masimulizi.<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu kudhibiti itikadi za kidini na za kijamii. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili hufundisha uandishi wa insha kama mojawapo ya stadi za lugha. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya masimulizi, tarakilishi yenye teknolojia saidizi,vifaa  vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1**<br><br>**Nyakati na Hali**<br><br>• *Hali ya mazoea (hu)*<br>• *Hali timilifu (me)*<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya hali ya mazoea na hali timilifu katika kitenzi,<br>b) kutambua vitenzi katika hali ya mazoea na hali timilifu katika matini,<br>c) kutumia vitenzi vya hali ya mazoea na timilifu katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>d) kufurahia matumizi ya hali ya mazoea na timilifu katika mawasiliano. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua viambishi vya hali ya mazoea (hu) na hali timilifu (me) kwenye vitenzi katika chati, ubao au kwa kutumia vifaa vya kidijitali yenye teknolojia saidia, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua viambishi vya hali ya mazoea (hu) na hali timilifu (me) kwenye orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vitenzi katika hali ya mazoea (hu) na hali timilifu (me) kwenye sentensi, chati, ubao au kwa kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vitenzi katika hali ya mazoea (hu) na hali timilifu (me) kwenye orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | Hali ya mazoea na timilifu hutofautiana kivipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ashiriki na wenzake katika mazoezi ya kutumia hali ya mazoea (hu) na hali timilifu (me) katika sentensi na kuziandika daftarini au kupiga chapa kwenye tarakilishi/kipakatalis*hi* chenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona ashiriki na wenzake katika mazoezi ya kutumia hali ya mazoea na hali timilifu kwenye karatasi za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wenzake katika vikundi kubadilisha sentensi kutoka hali moja hadi nyingine.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi katika hali ya mazoea na hali timilifu kwenye blogi ili wenzake waweze kuisoma na kutathmini usahihi wake. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za vikundi darasani na mtandaoni.<br>• Ubunifu: Mwanafunzi anapotunga sentensi.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoendelea kutunga sentensi katika hali ya mazoea na hali timilifu.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kipakatalishi au tarakilishi kutunga sentensi na vile vile kuzisambaza mtandaoni. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapojifunza kuthamini maoni ya wengine.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi. |

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Kujithamini na kujitambua: mwanafunzi anapotunga sentensi na kuzitumia kujieleza.<br>• Tamaduni hasi za kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi zinazohusiana na kudhibiti itikadi za kidini na za kijamii. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili pia hushughulikia matumizi ya nyakati na hali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Orodha maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

**11.0 UWEKEZAJI**

| **Mada** | **Mada ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **11.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **11.1.1 Masimulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kusikiliza masimulizi kwa kuzingatia ujumbe<br>b) kusimulia tungo mbele ya wenzake kwa kuzingatia mada, ubunifu na usanifu wa lugha,<br>c) kutumia ishara zifaazo kuimarisha masimulizi yake,<br>d) kuchangamkia masimulizi katika mazingira mbalimbali. | ● Mwanafunzi asikilize masimulizi yakitolewa na mgeni mwalikwa, mwalimu, mwanafunzi mwenzake au kutokana na vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona abuni masimulizi yanayohusiana na mada husika kwa kutazama picha, michoro au kujadiliana na wenzake, mwanafunzi asiyeona abuni masimulizi yanayohusiana na mada husika kwa kusikiliza maelezo ya picha, maelezo ya michoro au kujadiliana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona | Je, unazingatia mada kwa nini unapotoa masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | aelekezwe kubuni masimulizi yanayohusiana na mada husika kwa kutazama picha, michoro au kujadiliana na wenzake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kubuni masimulizi yanayohusiana na mada husika kwa kusikiliza maelezo ya picha na michoro au kujadiliana na wenzake<br>• Mwanafunzi atoe masimulizi kuhusu mada (*k.v.* *Jinsi ya kuwekeza na faida za uwekezaji.*<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atumie ishara za mwili zifaazo k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia ishara za mwili zifaazo k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi ajadiliane na wenzake kuhusu ubora wa masimulizi aliyosikiliza. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili kuhusu ubora wa masimulizi na wenzake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga na kusimulia visa mbalimbali.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposimulia visa mbele ya wenzake.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotoa masimulizi kuhusu uwekezaji.
- Umoja: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake ubora wa masimulizi aliyosikiliza.

**Masuala Mtambuko:**

- Elimu ya fedha: mwanafunzi anaposimulia kuhusu uwekezaji.
- Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anaposimulia kuhusu uwekezaji katika kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili linafunza kuhusu ufasaha wa kusema kwa ubunifu

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Picha, maelezo ya picha, michoro, maelezo ya michoro, mgeni mwalikwa

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.2 Kusoma** | **11.2.1**<br>**Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha,<br>b) kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu kwa kasi ifaayo,<br>d) kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo,<br>e) kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji. | ● Mwanafunzi aelekezwe kujadiliana na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame vielelezo vya video vinavyoonyesha usomaji fasaha wa makala (k.v. hotuba, habari,) akiwa peke yake au na wenzake, mwanafunzi asiyeona asikilize vielelezo vya video vinavyoonyesha usomaji fasaha wa makala (k.v. hotuba, habari,) akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu akizingatia matamshi bora.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha habari kwa kasi isiyopungua maneno 85 kwa dakika moja kuhusu suala lengwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe | 1. Je, kwa nini tunazingatia matamshi bora tunaposoma?<br>2. Unafanya nini ili kujua maana ya msamiati uliotumiwa katika kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kusoma kifungu akizingatia sauti ifaayo (k.v. kiwango cha sauti na kiimbo).<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo panapofaa (k.v. ishara za uso na mikono zinazozingatia tamaduni), mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu kwa kuambatanisha na toni inayofaa. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposoma kifungu au mchezo mfupi kwa sauti na kupishana nafasi na wenzake.<br>● Uwazaji wa kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojibu maswali kutokana na kifungu.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anaposoma kuhusu uwekezaji na jinsi ya kujikimu kimaisha. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anaposikiliza kwa makini wenzake wakisoma kifungu.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa ukamilifu. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu kwa maendeleo endelevu: mwanafunzi anapojifunza kuhusu elimu ya fedha hususan uwekezaji.<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapopata maarifa ya kujitegemea anapoandaa bajeti yake. |

| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English: somo hili linashughulikia mada ya kusoma vifungu vya ufahamu. |
|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kapu maneno, orodha maneno, mti maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, matini ya breli, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.3 Kuandika** | **11.3.1**<br>**Barua Pepe**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua baruapepe kwa kuzingatia muundo wake,<br>b) kuandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo,<br>c) *kuandika baruapepe kwa kutumia alama za breli za kuakifisha zifaazo (mwanafunzi asiyeona)*<br>d) kuchangamkia uandishi wa baruapepe katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua muundo wa baruapepe kwa kurejelea kielelezo chake kilichochapishwa au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili sehemu mbalimbali za baruapepe kama vile anwanipepe ya mtumaji *(k.m. tina18@gmail.com*), anwanipepe ya mpokeaji, mada ya baruapepe, mtajo, mwili, hitimisho na jina la mwandishi/ mtumaji.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika baruapepe kwa rafiki, mzazi, mwalimu n.k akishirikiana na wenzake darasani, kwa kutumia tarakilishi akizingatia muundo wa uandishi wa baruapepe.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika baruapepe | Je, barua pepe huandikwa vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwa rafiki, mzazi, mwalimu akishirikiana na wenzake kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi akizingatia muundo wa uandishi wa baruapepe, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika baruapepe kwa kutumia alama za breli za kuakifisha zifaazo k.m nukta, koma, herufi akishirikiana na wenzake kwa kutumia vifaa vya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akizingatia muundo wa uandishi wa baruapepe,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutuma baruapepe aliyoiandika kwa mpokeaji.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake kuhusu umuhimu wa baruapepe katika mawasiliano. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoandika na kutuma baruapepe.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika na kutuma baruapepe.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotuma baruapepe kwa mpokeaji.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapotuma baruapepe kwa wazazi au marafiki kuwajulia hali.
- Heshima: mwanafunzi anapozingatia maoni ya wengine wakati wa mijadala.

| |
|---|
| • Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza tarakilishi anayoitumia katika uandishi wa baruapepe. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Mawasiliano faafu: mwanafunzi anapotumia baruapepe kuwasiliana.<br>• Elimu kwa maendeleo endelevu: mwanafunzi anapotumia teknolojia kuwasiliana. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English**:** somo hili linashughulikia uadishi wa barua pepe |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha barua pepe, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.1 Ukanushaji**<br><br>*Viambishi vya wakati* ***li, na*** *na* ***ta***<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya wakati na nafsi katika sentensi,<br>b) kukanusha viambishi vya nafsi na wakati katika sentensi kwa usahihi,<br>c) kutunga sentensi sahihi zenye viambishi vya nafsi na wakati na kuzikanusha,<br>d) kufurahia ukanushaji wa viambishi vya nafsi na wakati katika sentensi. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua viambishi vya nafsi (*ni, tu, u, m, a, wa)* na vya wakati (*li, na, ta)* katika vitenzi kwa kuvipigia mistari kwenye vitabu vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza au kuvikolezea wino kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua viambishi vya nafsi (*ni, tu, u, m, a, wa)* na vya wakati (*li, na, ta)* katika vitenzi na aviandike kwenye karatasi za breli akizingatia alama za breli za mikato.<br>● Mwanafunzi aelekezwe *ku*tambua viambishi vya wakati ***li***, ***na***, ***ta*** katika hali yakinishi na ***ku, ta, si, ha,*** katika hali kanushi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma sentensi zenye | 1. Viambishi vya nafsi katika vitenzi ni muhimu, kwa nini?<br>2. Viambishi vya wakati katika vitenzi hutumiwa vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | viambishi lengwa kwenye vitabu au tarakilishi katika hali yakinishi na kanushi.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kukanusha sentensi akizingatia nafsi na nyakati kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au wenzake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kukanusha sentensi akizingatia nafsi na nyakati kwenye karatasi za breli au kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona asikilize au atazame vipindi vya ukanushaji wa nafsi na wakati kupitia vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au katika kikundi, mwanafunzi asiyeona asikilize vipindi vya ukanushaji wa nafsi na wakati kupitia vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au katika kikundi.. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapokanusha sentensi akizingatia viambishi vya nyakati husika akiwa na wenzake.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapokanusha sentensi akizingatia viambishi vya nyakati husika.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza au kutazama vipindi vya ukanushaji.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anaptunga sentensi katika hali Kanushi akizingatia viambishi vya nyakati **li**, **na** na **ta** |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini wenzake wanapotambua viambishi vya wakati li, na na ta katika hali yakinishi na ku, ta, si, ha katika hali kanushi.<br>● Uadilifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu uwekezaji. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Kujithamini: mwanafunzi anakuza uwezo wa kukabili au kukataa mambo mbalimbali maishani.<br>● Umaskini: mwanafunzi anapotumia viambishi vya nafsi na vya wakati katika sentensi zinazolenga suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English: somo hili pia hushughulikia viambishi vya nyakati na ukanushaji wake. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.2**<br>**Ukubwa na udogo wa nomino**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi mbili,<br>b) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** katika hali ya ukubwa na udogo,<br>c) kubadilisha nomino katika hali ya wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo,<br>d) kutumia nomino zinazoanza kwa herufi **m-** katika hali ya ukubwa na udogo kwenye sentensi,<br>e) kufurahia kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi mbili *(k.m mtoto, mlango, mkate na mlima)* kwenye chati, ubao, mti maneno, kapu la maneno au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi mbili *(k.m mtoto, mlango, mkate na mlima)* kwenye ordha maneno, kadi za breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi mbili katika ukubwa na udogo (k.v. mtoto (toto- kitoto), mlango (lango - kilango), mkate (kate- kikate).<br>● *Mwanafunzi* ashiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa na udogo.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika mchezo wa vikundi ambapo kikundi kimoja kitataja wastani wa nomino na kingine kutaja ukubwa na udogo wa nomino hiyo.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona apewe orodha ya nomino katika hali ya ukubwa na orodha nyingine ya nomino katika hali ya udogo kwenye tarakilishi ili aziburure | Ni nomino gani unazoweza kutaja ukubwa wake? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuziambatanisha, mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya nomino katika hali ya ukubwa na orodha nyingine ya nomino katika hali ya udogo kwenye tarakilishi na aziandike.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi zinazorejelea nomino lengwa katika ukubwa na udogo akiwa peke yake au kwenye vikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki mijadala kuhusu nomino katika ukubwa na udogo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi katika hali ya ukubwa na udogo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kutambua na kuambatanisha nomino katika hali ya wastani, ukubwa na udogo.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapofanya kazi katika makundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi za vikundi kwa utulivu.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotunga sentensi za ukubwa na udogo kuhusu uwekezaji.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili pia hushughulikia ukubwa na udogo wa nomino.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Chati, ubao, mti maneno, kapu la maneno, kadi za breli, orodha maneno, kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.3** **Ukubwa na udogo wa nomino** <br><br> (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze: <br> a) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **n-** ili kuzitofautisha na nonimo nyingine, <br> b) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **n-** katika hali ya ukubwa na udogo, <br> c) kubadilisha nomino katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo, <br> d) kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwenye sentensi ili kuimarisha mawasiliano, <br> e) kufurahia kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwa usahihi ili | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **n-** kwenye chati, ubao, mti maneno, kapu la maneno au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi n kutoka kwa orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. <br> ● Mwanafunzi ashiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa na udogo. <br> ● Mwanafunzi ashiriki katika mchezo wa vikundi ambapo kikundi kimoja kitataja wastani wa nomino, kingine ukubwa na kingine kutaja udogo wa nomino hiyo. <br> ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona apewe orodha ya nomino katika hali ya ukubwa na orodha nyingine ya nomino katika hali ya udogo kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na | Je, tunatambua vipi ukubwa na udogo wa nomino? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuimarisha mawasiliano. | aelekezwe kuziburura na kuziambatanisha, mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya nomino katika hali ya ukubwa na orodha nyingine ya nomino katika hali ya udogo kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na aelekezwe na kuziambatanisha kwa kuziorodhesha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi zinazorejelea nomino lengwa katika ukubwa na udogo akiwa peke yake au kwenye vikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki mijadala kuhusu mada hii
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi katika hali ya ukubwa na udogo.

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kutambua na kuambatanisha nomino katika hali wa wastani na udogo

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anaposhiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa na udogo.
- Umoja: mwanafunzi anapotunga sentensi katika ukubwa na udogo akiwa kwenye vikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Upendo: mwanafunzi anaposhiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa na udogo.
- Umoja: mwanafunzi anapotunga sentensi katika ukubwa na udogo akiwa kwenye vikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**
English: somo hili pia hushughulikia ukubwa na udogo wa nomino.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Orodha maneno,kadi maneno,mti maneno,tarakilishi yenye teknolojia saidizi.

**MWONGOZO WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA**

**MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuwasiliana kwa kuzingatia matamshi bora** (*matamshi ya sauti zinazokaribiana: f/v,s/z,l/r,th/dh*) | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti 7 – 8 zilizolengwa . | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti 5-6 zilizolengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti 3-4 zilizolengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti 1- 2 zilizolengwa. |
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha** *(maneno ya udugu: bwana, bibi, binti, mama, mama mkubwa/mdogo, mjomba)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia maneno 6-7 ya udugu katika miktadha mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akitumia maneno 4-5 ya udugu katika miktadha mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akitumia maneno 2-3 ya udugu katika miktadha mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akitumia neno 1 la udugu katika baadhi ya miktadha. |
| **Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo** **(***maamkuzi na maagano ,mazungumzo ya kimuktadha*) | Anasikiliza na kujibu maamkuzi na maagano kwa kuzingatia miktadha ifaayo kwa wepesi. | Anasikiliza na kujibu maamkuzi na maagano kwa kuzingatia miktadha ifaayo | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi na maagano kwa kuizingatia miktadha ifaayo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi na maagano na kuzingatia baadhi ya miktadha ifaayo kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutumia lugha kiubunifu** *(vitendawili, methali, ushairi, nahau, visawe,tashbihi na masimulizi)* | Anazungumza kwa kuzingatia vipengele 6-7 vya lugha ya kiubunifu. | Anazungumza kwa kuzingatia vipengele 4-5 vya lugha ya kiubunifu. | Anazungumza kwa kuzingatia vipengele 2-3 vya lugha ya kiubunifu. | Anazungumza kwa kuzingatia kipengele 1 cha lugha ya kiubunifu. |

**MADA: KUSOMA**

| Vigezo \ Viwango | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu - Vifungu/mashairi/ maigizo** *(ujumbe,matumizi ya msamiati mwafaka,wahusika,matukio na kutoa muhtasari)* | Anasoma vifungu, mashairi na maigizo na kutambua 5 vipengele husika. | Anasoma vifungu, mashairi na maigizo na kutambua vipengele 3-4 husika. | Anasoma vifungu, mashairi na maigizo na kutambua vipengele 2 husika. | Anasoma vifungu, mashairi na maigizo na kutambua kipengele 1 husika. |
| **Kuweza kusoma kwa kina.** *(Matumizi ya kamusi: mpangilio, maana za maneno na utumizi wa maneno)* | Anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio, maana na utumizi wa maneno kwa urahisi. | Anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio, maana na utumizi wa maneno. | Anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio na maana ya maneno. | Anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio maneno. |
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.** (*matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo*) | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 4 vya kusoma kwa ufasaha kikamilifu. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 3 vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 2 vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia kipengele 1 cha kusoma. |
| **Kuweza kusoma kwa mapana.** *(kutambua na kuchagua makala ya kusoma, kutambua ujumbe na matumizi ya lugha)* | Anasoma makala ya kujichagulia na kutambua ujumbe na matumizi ya lugha kwa wepesi. | Anasoma makala ya kujichagulia na kutambua ujumbe na matumizi ya lugha. | Anasoma makala ya kujichagulia na kutambua kwa kiasi ujumbe na matumizi ya lugha. | Anasoma makala ya kujichagulia na kutambua kwa ujumbe. |
| **Kuweza kusoma kidijitali.** **(***kuzingatia hatua za kiusalama katika kutumia vifaa vya kidijitali, kufungua faili, kusakura matini kwenye tovuti salama.)* | Anasoma matini ya kidijitali akizingatia vipengele 3 vifaavyo kwa uketo. | Anasoma matini ya kidijitali akizingatia vipengele 3 vifaavyo. | Anasoma matini ya kidijitali akizingatia vipengele 2 vifaavyo. | Anasoma matini ya kidijitali akizingatia kipengele 1 ifaavyo. |

**MADA: KUANDIKA**

| Viwango / Vigezo | Kuzidi matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha** (*wasifu, masimulizi, maelezo)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe na mtindo. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele 3 vifaavyo vya uandishi kwa utendeti. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele 3 vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele 2 vifaavyo vya uandishi. | Anaandika insha kwa kuzingatia kipengele 1 kifaacho cha uandishi. |
| **Kuweza kutambua na kutumia sehemu za tarakilishi, kuandika baruapepe.** *(Muundo, ujumbe na mtindo).* | Anaandika baruapepe kwa tarakilishi kwa kuzingatia vipengele 3 vifaavyo kwa uketo. | Anaandika baruapepe kwa tarakilishi kwa kuzingatia vipengele 3 vifaavyo. | Anaandika baruapepe kwa tarakilishi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele 2 vifaavyo. | Anaandika barua pepe kwa tarakilishi kwa kuzingatia kipengele 1 kifaacho. |

**MADA: SARUFI**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kutambua na kutumia aina mbalimbali za nomino katika lugha ya Kiswahili.<br>(nomino za pekee, kawaida,wingi, vitenzi jina,makundi,ambata na dhahania*)* | Anatambua na kutumia aina 6-7 za nomino katika matini kwa kina. | Anatambua na kutumia aina 4-5 za nomino katika matini. | Anatambua na kutumia aina 2-3 za nomino katika matini. | Anatambua na kutumia nomino 1 katika matini. |
| Kuweza kutambua na kutumia alama za uakifishi.<br>*(herufi kubwa,koma,kikomo na kiulizi)* | Anatambua na kutumia alama 4 za uakifishi katika matini. | Anatambua na kutumia alama 3 za uakifishi katika matini. | Anatambua na kutumia alama 2 za uakifishi katika matini. | Anatambua na kutumia alama 1 ya uakifishi katika matini. |
| Kuweza kutambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo.<br>(I-ZI, U-ZI, U-YA, KU-KU) | Anatambua viambishi vya ngeli 4, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | Anatambua viambishi vya ngeli 3, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | Anatambua viambishi vya ngeli 2, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | Anatambua viambishi vya ngeli 1, ngeli za nomino na kutumia kwa kiasi upatanisho wa kisarufi ipasavyo. |
| Kuweza kutambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali.<br>*(kutendewa,<br>kutendeka na kutendana)* | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli 3 za mnyambuliko wa vitenzi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli 2 za mnyambuliko wa vitenzi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli 1 ya mnyambuliko wa vitenzi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli 1 ya mnyambuliko wa vitenzi kwa kutatizika. |
| Kuweza kutambua vinyume vya vitenzi na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya vitenzi 5 na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya vitenzi3- 4 nakuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya vitenzi 2 na kuvitumia katika matini. | Anatambua kinyume cha kitenzi 1 na kukitumia katika matini. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kutambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali kwenye matini.<br>*(hu-* na - *me-)* | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali kwenye matini kwa utendeti. | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali kwenye matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya nyakati na hali kwenye matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya nyakati na hali kwenye matini kwa kuongozwa. |
| Kuweza kutambua viambishi vya ukanushaji katika hali ya mazoea na hali timilifu.<br>*(hu-* na - *me-)* | Anatambua viambishi vya ukanushaji katika hali ya mazoea na hali timilifu kwa wepesi. | Anatambua viambishi vya ukanushaji katika hali ya mazoea na hali timilifu. | Anatambua baadhi ya viambishi vya ukanushaji katika hali ya mazoea na hali timilifu. | Anatambua baadhi ya viambishi vya ukanushaji katika hali ya mazoea na hali timilifu kwa kutatizika. |
| Kuweza kutambua na kutumia viambishi vya wakati na nafsi katika sentensi na kuzikanusha<br><br>(*Viambishi vya wakati li, na* na *ta)* | Anatambua na kutumia viambishi vya wakati na nafsi katika sentensi na kuzikanusha kwa wepesi. | Anatambua na kutumia viambishi vya wakati na nafsi katika sentensi na kuzikanusha. | Anatambua na kutumia viambishi vya wakati na nafsi katika baadhi ya sentensi na kuzikanusha. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya wakati na nafsi katika sentensi na kukanusha baadhi ya sentensi. |
| Kuweza kutambua nomino katika hali ya ukubwa na udogo<br>*(nomino zinazoanza kwa kiambishi m-* na *kiambishi n-)* | Anatambua na kutumia nomino 5 katika hali ya ukubwa na udogo kwa wepesi. | Anatambua na kutumia nomino 3-4 katika hali ya ukubwa na udogo. | Anatambua na kutumia nomino 2 katika hali ya ukubwa na udogo. | Anatambua na kutumia nomino 1 katika hali ya ukubwa na udogo. |

## KIAMBATISHO 1: MWONGOZO WA MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI KATIKA GREDI YA 4-6

### UTANGULIZI

Katika kiwango hiki, lengo la shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji ni kupata uwiano kati ya dhana zilizofunzwa katika masomo mbalimbali na maisha ya kila siku. Wanafunzi wanafanya ulinganisho kati ya kile wamejifunza na maisha yao ya kila siku. Shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji imeshughulikiwa katika somo la *Social studies*. Utekelezaji wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji inahitaji ushirikiano ambapo mwalimu anashirikiana na walimu wa masomo mengine kuandaa na kutekeleza shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Ingawa shughuli hizi zinaelekezwa na mwalimu, mwanafunzi anatakiwa kupewa nafasi ya kutambua changamoto/tatizo na kuzua utatuzi wake. Usalama wa mwanafunzi unatakiwa kuzingatiwa katika utambuzi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Hatua zifuatazo za shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji zinatakiwa kusambazwa katika mihula yote**.**

| **Hatua za utekelezaji wa shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji** |
|---|
| **1) Maandalizi**<br>● Tambua umilisi wa kimsingi unaolengwa, maadili na stadi zinazokusudiwa katika matokeo maalum yanayotatarjiwa kwa mujibu wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji.<br>● Tambua nyenzo hitajika katika shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji (zinazopatikana katika mazingira)<br>● Kusambaza shughuli hizo katika muhula mzima (bainisha siku na wakati/muda wa shughuli hizo).<br>● Wasiliana na wanafunzi, wazazi/walezi, wasimamizi wa shule, walimu na washikadau wengine katika jamii ya shule.<br>● Tambua na kuandaa vifaa vya tathmini. |

| |
|---|
| 2) **Utekelezaji wa Shughuli Jumuhishi ya Huduma ya Jamii.**<br>● Gawia wanafunzi majukumu.<br>● Hakikisha kila mwanafunzi anashriki kikamilifu katika shughuli husika.<br>● Tazama wanafunzi wanapotekeleza shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji na kurekodi matokeo ya utekelezaji wao.<br>● Tumia kifaa cha tathmini kinachofaa kutathmini mchakato mzima pamoja na matokeo yake (tathmini kazi ya mwanafunzi kuanzia mwanzo hadi mwisho).<br>● Tathmini umilisi wa kimsingi unaolengwa, maadili na stadi katika somo. |
| **3) Tafakuri kuhusu Shughuli ya Huduma Jumuhishi ya kijamii.**<br>Chukua nafasi ya kujitathmini kuhusu shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji ukiwa na wanafunzi kwa kujadiliana nao kuhusu yafuatayo:<br>● Ni nini kilifanyika vizuri na kwa nini<br>● Ni nini hakikufanyika vizuri na kwa nini<br>● Ni nini kinaweza kufanywa tofauti<br>● Wamejifunza nini |

Kutakuwa na shughuli moja jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji itakayotekezwa mara moja kwa mwaka. Masuala ya shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji yatatokana na masuala mtambuko pana katika masomo tofautitofati. Waalimu wanatakiwa kuangazia suala tofauti kila mwaka ili kuwapa wanafunzi fursa ya kushughulikia masuala mtambuko mbalimbali katika miktadha yao.

Shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji itashirikisha kila mmoja katika jamii ya shuleni (wanafunzi, wazazi/zalezi, wasimamizi wa shule na walimu). Wazazi/walezi ni washikadau muhimu katika maandalizi na utekelezaji wa shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Ingawa walimu wana jukumu muhimu katika maandalizi na ujumuishaji wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji, wanafunzi wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima.
Shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji inampa mwanafunzi nafasi ya kukuza umilisi wa kimsingi na maadili mbalimbali. Mwalimu anatakiwa kubadilisha umilisi wa kimsingi na maadili yanayoangaziwa kila mwaka.

**Tathmini ya shughuli Jumuhishi ya Huduma ya Jamii.**

Tathmini ya Shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji itaangazia vipengele vitatu ambavyo ni: stadi katika masomo mbalimbali yaliyoshirikishwa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji, umilisi wa kimsingi na maadili yanayodhihirishwa. Ni lazima tathmini izingatie mchakato mzima pamoja na matokeo ya shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Mwalimu atawatathmini wanafunzi wakiwa katika vikundi akitumia vifaa vya tathmini kama vile ratiba ya ukaguzi, orodha hakiki, viwango vya ukadiriaji au kifaa kingine kinachafaa.

**KIAMBATISHO 2: MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI**

| **Mada** | **Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini** | **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia** | **Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji** |
|---|---|---|---|
| KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>e) Kuambatanisha maneno na majibu<br>f) Mijadala<br>g) Mazungumzo<br>h) Matumizi ya ishara za mwili k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>i) Wanafunzi kufanyiana tathmini | • Chati<br>• Michoro na picha au maelezo ya michoro na picha<br>• Mgeni mwalikwa<br>• Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>• Mti maneno au orodha maneno<br>• Kapu maneno<br>• Vitabu mbalimbali vyenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza/ vitabu vya breli | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| KUSOMA | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa<br>b) Kujibu maswali k.m. katika ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kukariri na kuimba mashairi<br>e) Kusoma kwa sauti<br>f) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>g) Potfolio<br>h) Shajara | • Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu yenye teknolojia saidizi<br>• projekta<br>• Nakala ya shairi<br>• Kamusi mbalimbali | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| **Mada** | **Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini** | **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia** | **Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji** |
|---|---|---|---|
| KUANDIKA | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potfolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | • Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Kielelezo cha insha ya wasifu<br>• Nakala ya barua ya kirafiki<br>• Nakala ya barua rasmi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| SARUFI | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno lengwa<br>c) Kujaza nafasi<br>d) Kujaza fumbo maneno<br>e) Kazi mradi | • Tarakilishi/vipakatalishi yenye teknolojia saidizi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• Projekta<br>• Kapu maneno au orodha maneno<br>• Mti maneno<br>• Kadi za maneno<br>• Kadi za breli<br>• Picha au maelezo ya picha ya vitu mbalimbali<br>• Michoro au maelezo ya michoro<br>• Chati<br>• Mabango<br>• Sanamu<br>• Nyenzo halisi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Ziara za nyanjani<br>4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali yenye teknolojia saidizi |